

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**Verbatim Report Of**

**DISSEMINATION OF REPORT & DRAFT BILL**

**COAST PROVINCE, KALOLENI CONSTITUENCY**

**AT KALOLENI SOCIAL HALL**

**ON**

**7<sup>TH</sup> OCTOBER 2002**

**DISSEMMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, KALOLENI CONSTITUENCY, HELD AT KALOLENI SOCIAL HALL**

**Present :**

Com. Mohamed Swazuri

**Secretariat:**

Verbatim Recorder - Lydia Moraa  
District Co-ordinator - Daniel Mwaringa

**The meeting started at 11.09 a.m with prayers from Stephen Ngumbao and Dr. Swazuri in the Chair.**

**Daniel Mwaringa :** Haya, watu wa Kaloleni mmeamkaje. Nashukuru kuona watu wote ambao wamefika hapa ili tuendeshe hii shuguli ambao mmeisikia kuhusu launching ya hii Draft Constitution. Lakini kwanza kabisa kabla hatujawapatia maelezo mengine tungetaka tupate mtu atufungulie kwa maombi, halafu nitawaelezea ile ratiba iko vipi nitawajulisha nani yuko hapa na kwa nini hata tuko hapa na mathumuni yetu na mazungumzo mengine yote yatafwata. Kwa hivyo tungetaka tupate mtu

atufungulie kwa maombi tafadhali.

**Stephen Ngumbao :** Haya tuombe: Mwenyezi Mungu Baba tunakutolea sifa na shukurani kwa siku ya leo sababu ya mapenzi yako yaliyo makuu yapate kutuwezesha kuwa katika kongomano hili ambapo Bwana tuna shuguli muhimu ambapo bila wewe hatuwezi. Hata hivyo tunaomba usaidizi kutokana kwako ukapate kutubariki na kutufanikisha nia zetu na mawazo yetu ili kwamba tukapate kuleta maendeleo katika nchi hii ya Kenya. Bariki kila mmoja ambaye anahusika na jambo hili na tunaomba haya tukijua umetusikia na utatenda na ni kwa jina la Yesu aliye Bwana mkuu, tunaomba tukiamini. Amina.

**Daniel Mwaringa :** Asante sana kwa wale ambao pengine walikuwa hawajafanya registration, tafadhali hakikisha kabla hujaondoka uwe umejiandikisha katika ile orodha pale ili tujue ni kina nani walikuja tuweze kufanya hiyo data. Jambo lingine ambalo ningetaka kusema ni kwamba mambo mengi yatazungumzwa na Commission wetu hapa ambaye nataka niwajulishé kwenu. Commissioner Dr. Mohamed Swazuri, yeye ndio yuko hapa kuzungumza na sisi khuhusu jambo hili la Katiba ile draft ambaye imetoka na pia tuko na Secretariat staff yetu hapa ingine. Madam hebu uwajulishé jina lako.

**Lucy Awasi :** Mimi naitwa Lucy Awasi,

**Daniel Mwaringa :** Asante sana na hapa niko na Lydia Moraa. Mimi ni Coordinator wenu tumekutana mara kwa mara katika shuguli hizi, hizi za Katiba, naitwa Daniel Mwaringa.

Kwa hivi sasa nafikiri kulikuwa kuna kile kipindi ambacho wote tulikuja katika jengo hili, hili kikao hiki hiki tukatoa maoni yetu tofauti tofauti yale tuliotaka ama yale tuliyo pendekezo katika Katiba. Maoni yale yaliweza kujukuliwa katika sehemu zote za uakilishi bungeni 210 katika jumuiya yetu ama Republic yetu na baadaye wakaketi hawa Makamishna wakaweza kuyatondona na kuweza kuyatoa katika ripoti kadha, kadha nakutoa mswada ambayo hivi leo Doctor Mohamed Swazuri, Commissioner wetu atau-launch officially katika Constituency hii yetu ya Kaloleni. Kutakuwa na mazungumzo kadha kadha halafu tutaweza kuchangia ama kuongezea lolote lile ambalo tunaona pengine ni la umuhimu katika Katiba hii.

Pengine ningetaka kusema Commissioner tafadhali usione nachukua muda mrefu. Ningetaka kusema kwamba msione kwamba hii draft ndio Katiba imetoka, hii ni proposal, kwa hivyo msije mkatoka hapa mkasema Katiba tayari tuko nayo. Huu mswada ni proposal tu ambazo zimefanywa na Tume ya marekebisho ya Katiba kulingana na yale maoni ambayo mulitoa, ili tuweze kujadiliana katika kipindi cha wiki tatu, wiki nne na leo si mwisho leo ni ku-launch tu halafu tutapanga na kina, hawa sisi wetu vile tutapokwenda kule kwa mukutano na hasa makundi tofauti ili kuzungumzia saidi ya mswada huu. Halafu tutapata lile fungamano la National Constitutional Conference ambapo tayari tushachagua delegates, tulikuwa na election na delegates wakachaguliwa na nafiri pia Ma-Councillor mulikuwepo mkapiga kura hii. Kwa hivyo nafikiri kufikia hapo ndio kazi ya tume, tutaendelea zaidi katika kuzungumza kwetu. Commissioner tafadhali. Asante.

**Com. Swazuri :** Asante sana Bwana Maringa habari za asubuhi. Nafikiri sasa mimi si mgeni hapa. Kwanza tunawashukuru wale ambao wamefika na tunatumaini wengi wataendelea kufika ili kufanikisha mjadala wa leo. Kama alivyosema Bwana Co-ordinator, sisi tumekuja hapa leo kwa kufwata sheria. Sheria ilituambia baada ya kukusanya maoni yenu na kuandika ripoti yetu ni lazima tuirudishe tena kwenu ninyi wananchi. Tuwapatie muiangalie halafu mue na nafasi ya kusema kwamba hivyo ndivyo, tufanye nini ndio sababu ambayo imetuleta hapa. Kama tungekuwa na wakati ingekuwa na kila mmoja apatiwe na kala na ule Mswada wa Katiba kabla ya leo kila mtu auchunguze auangalie halafu leo tukikutana hapa ndio kila mtu aweze kusema mimi nina swali kuhusu kifungo fulani, nilikuwa nataka hivi, mbona iko hivi? Lakini kwa sababu ya wakati umekuwa ni kidogo, halafu nakala ambazo zilikuwa zinatakikana kuchapishwa ni nyingi mno, halafu hatukwa na wakati wa kuwapatia watu wakutafsiri Kiswahili, kwa hivyo ile nakala ya Kiswahili pia hatuna hapa tulio nayo ni ya Kingereza. Kwa hivyo kidogo tutakuwa na watu kusitasita maana yake wengine hawataufikia ule Mswada.

Lakini kama aliposema Bwana Co-ordinator baada ya sisi tumekuja hapa kuwafungulia mjadala na nina ruhusa ya kuzungumza. Ninyi wenyewe mtaitwa kwenye mikutano ambayo kila mtu atakuwa kuanzia leo amepata Nakala yake akasome halafu mtaandika yale ambayo mnafikiria yafanywe marekebisho au kama yote ni sawa pia tutataka kusikia halafu hao yataletwa tena kwetu kwa Tume ili kuhakikisha ya kwamba tumekusanya maoni ya kila mtu. Na baada ya shuguli hiyo ya kutoa maoni yenu, tena tutaandika yale marekebisho halafu tuwarudishie kwenya National Conference.

Tutakuwa na mkutano wa Kongamano la kitaifa la wananchi wale ambao wamachaguliwa. Wale tuliyosema 650 watacaa kwa mwezi mmoja tukijaliwa kuanzia 28<sup>th</sup> ya Mwezi huu, Nairobi, Bomas of Kenya. Hawa wanatakikana waende kama hivi ambao tutafanya kifungo baada ya kifungo, wakubaliane waende kifungo kingine wakubaliane mpaka mwisho kwa mwezi mzima. Wacha hi yetu ni ya siku moja, hiyo yao ni ya mwezi mzima. Halafu wakimaliza hapo ndio tutapelika Bunge ili iweze kuitisha. Hayo ndio mathumuni haswa yakatuleta hapa ni jukumu katika sheria ya kurekebisha Katiba.

Kwa hivyo wale ambao hawana, ungewapatia, wale ambao hawana, mbao wanaweza kusoma Kingereza, ile ya Kiswahili tutaileta. Hii wiki haitoisha tutaileta ya Kiswahili kwa hivyo kama huwezi soma Kingereza usishaushiwe na haja ya kuchukua tutakusomea kwa Kiswahili halafu ile ya Kiswahili itafika. Watu wengine wanachukua tu kwenda kuweka bila ya kuifanyia kazi haijafika ile ya kuchukuwa na kuweka hii bado ni ya kufanya kazi. Kwa hivyo ukachukua kwenda kuiweka ika badilishwa yote ikawa wewe sasa wewe umechuwa karatasi haukuchukua Swale. Kwa hivyo watu wasifanye pupa ya kwamba lazima wachukue yejote waweka nyumbani, ah, ah, bado. Moja moja tu wala usiseme kwamba yule mwenzangu, rafiki yangu nyumbani awa bwanangu amenituma ah, ah. Kwa sababu hasitoshi.

Haya natumaini kila mtu, wale ambao wanaweza kuelewa Kingereza kila mtu ana nakala yake na wale ambao wanaweza kusoma magazeti katika wiki mbili hivi na kusikiliza vyombo via habari, mambo mengine yamesemwa.

Katiba yenewe tunayo itarajia itakuwa na chapters ishirini, 20 chapters. Tutakuwa na vifungu saidi ya mia mbili. Tutakuwa na

vifungu mia mbili tisini na tisa karibu mia tatu. Na tumefanya kama vile wananchi walisema tumejari bado twaendelea kufanya, kurahisisha lugha katika huu Mswada, ukiangalia sana ile lugha ya kisheria kidogo imepungua. Yaani mambo ya Kilatinin yale tumeyatoatoa. Lakini bado tumeacha wenzetu Nairobi wanajaribu kuirahisisha hii lugha ya hii Katiba. Bado iwe rahisi saidi. Kuna maneno bado ya kisheria ambayo yanatatiza watu hapa na kila ukiliona pia neno hilo unaweza ukalipiga mustari ukatuambia maneno haya hayaeleweki kwa urahisi bado tunaendelea kuifanya iwe rahisi saidi.

Halafu tulikuwa na mjadala kuhusu urefu au wingi wa hii Katiba, wengine walisema hatutaki Katiba ndefu sana wengine wakasema tunataka Katiba iwe ndefu sasa tumejaribu isiwe kubwa sana isiwe ni kitabu mtu akibeba asikie uzito au isiwe kikaratasi tu ambacho mtu anaweza kujifungua maamri akaenda zake kwa hivyo iko katikati ya hapo. Si kubwa, wale si ndogo ili kila mtu aweze kunufaika nayo.

Kwa hivyo kwanza, tutazungumzia, nitawaeleza zile tofauti zilizoko baia ya Katiba hii na Katiba tuliyo nayo sasa, ile ambayo tunairekebisha. Kitu cha kwanza kama tulivyo ahidi hapo mwanzo Katiba hii ni kweli imetengenezwa na wananchi, sio Katiba ya watu fulani kwenda kukaa mahali na kuandika, haya ni maoni ya wananchi. Kila unalo liona pale tumeongeza uchuzi wetu tu ya kwamba ni sehemu zipi, lakini ni la wananchi. Hakuna hata kifungo kimoja hapa ambacho kimefikiriwa tu kikawekwa. Kila kifungu tumekijadili kutokana na maoni ya wananchi.

Halafu pili, Katiba hii iko na Preamble utangulizi ambapo wananchi wengi walisema wanataka utangulizi maana yake Katiba ya zamani au hii ya sasa tuliyo nayo haina utangulizi, hiyo ni tofauti ingine.

Halafu haki za binadamu za binadamu zilikuwa hazikutiliwa mkazo kwenye Katiba ya zamani lakini Mswada wetu hapa una vifungu karibu hamsini, ilivyofwatana. Ukiangalia Chapter 5 Bill of Rights. Hizo ni haki za kimsingi, haki za kibinadamu karibu zimechukua vifungu hamsini. Hiyo ni tofauti kubwa kabisa.

Halafu jambo nyingine Katiba hii inasingatia umuhimu was wananchi katika uongozi, good governance, participation in good governance unazingalia wananchi wamehusishwa katika kusimamia maisha yao. Siyo kama pale samani ambapo ilikuwa Serikali ndio inasimamia kila kitu. Katika Katiba hii tumejaribu kuhahakikisha kwamba wananchi wanajisimamia.

Katika upande wa mambo au mambo ya uchaguzi Katiba hii imehahakisha kwamba sio lazima uwe mwanachamawa chama fulani ndio ukombee uchaguzi, siyo lazima. Independent candidates Wanaruhusiwa, katika ngazi zote si lazima uwe mwanachama wa chama fulani.

Tofauti pia ya Katiba hii ni kwamba vyama vya kisiasa vile ambavyo vina nguvu , vitawenza kupata pesa kutoka kwa Serikali. Vile ambavyo vina nguvu lakini siyo vyote 49 sijui 48, vile ambavyo vitakuwa vina nguvu na zile nguvu tumesitaja, ambavyo vitakuwa vimeshinda viti number fulani, vitakuwa na rukza ya kupatiwa pesa.

Pia tumetaja safari, kazi za vyama vya kisiasa ni nini. Katiba ya sasa yaina hiyo. Tumesam a kazi za vyama via kisiasa inatakikana vifanye kadha kadha, ndio vifike katima maendeleo hata kama haviko Bunge na chama kisicho fanya kazi zile automatically kinakuwa deregistered maana yake hakijafanya kazi zake. Kwa hivyo tumetoa jukumu responsibility kwa vyama, visiye tu vinakaa miaka mitano vinangojea wakati wa uchaguzi ndio vinaamka. Kikifanya hivyo hasibaki pesa. Na kama hakina pesa kitakufa. Hiyo ni tofauti ingine ambayo tumeiweka.

Tofauti ingine tumeipatia Bunge nguvu saidi, na mamlaka kuliko ilivyokuwa zamani. Itakuwa na mamlaka kuliko hivi sasa mamlaka ya kangalia vitendo vya viongozi vya utawala, viongozi wa Serikali, yaani Rais, Prime Minister, Waziri Mkuu na wale viongozi wote wakuu wa mashirika wote watakuwa wanaangaliwa sana na Bunge. Tumesama kwamba Bunge ndio litataua, ndio litapitisha Rais anaweza kuteua au Waziri Mukuu anaweza kuteua lakini Bunge ndio mambo yote ndio linahakikisha. Hata kufuta kazi, sasa wale viongozi tumesema siyo kazi ya Rais hiyo atapendekeza tu kwamba fulani hafai halafu, itaenda Bunge waulize hafai vipi? Aeleze wale wakisema huu ni upuzi yule mtu ataendelea na na kazi. Habari ya kungojea habari za saa saba mchana, either uandikwe kazi au ufutwe kazi, sasa tumeondoa hiyo ni tofauti moja ambayo tumeiweka.

Tumesema pia katika Katiba hii mishahara ya viongozi wa uma, mashirika ya uma yatakuwa na Tume maalum ya kuangalia itakuwa si halali kwa viongozi au wabunge kuweka mishahara yao. Kuamua kwamba kuongeza laki sita ah, ah hiyo tumeondoa kwa sababu Katiba ya sasa inasema wanaweza, sisi tofauti yetu ni kwamba tumesema haiwezekani. Tumeunda Tume ya mishahara ya uma, yote mishahara yote, bora wewe mfanya kazi wa uma, wakuchaguliwa, wakuteuliwa lakini mishahara yenu itaangaliwa na Tume na hii Tume ina watu, mpaka wanachi wa chini, tumeweka nafasi zao. Wale wakae ndio waamue mshahara wa Bunge, mshahara wa Councillor, mshahara wa nani mshahara wa waziri, mshahara wa kuwa kilindini, mshahara wa nani itakuwa ni hiyo. Hiyo ni tofauti ingine ambayo tumeiweka.

Tofauti ingine ni kuhusu uraia. Tumeeleza vizuri kabisa raia wa Kenya ni nani unapatikanaje uraia na unamatizikaje uraia wa Kenya, tumeweka hiyo.

Halafu tukirudi tena kwa viongozi tunasema kwamba katika Katiba ya sasa kuna ruhusa wananchi kumkataa kiongozi waliyemuchagua, iko ruhusa hiyo na tumeeleza wananchi watafanya nini ili wamtoe yule kiongozi? Kutoka kiongozi anayechaguliwa katika kila ngazi mpaka Rais. mpaka Waziri Mkuu, mpaka Mbunge, mkisema kwamba huyu hafai kuna taratibu tumeziweka pale mnazifwata, huyu anatolewa. Kwa sababu kwamba hiyo ni njia moja ya fitina tumeweka vikwazo pale sababu tungeiacha loose hivi tungefanya uchaguzi kila siku. Maana yake kama watu wengine wana nguvu ya pesa za kuwaonga nyote mkatia saini akatolewa wiki iiao mwengine tena akatolewa, mwezi ujao mwengine mwengine akatolewa, hivyo tu lakini tumeweka vikwazo, kama hafai kweli basi asilimia sitini na sita wale waliomchagua wakubali kwamba hafai hapo ndio tutamtoa. Hiyo ni tofauti ingine ambayo tumesema.

Katika Katiba hii pia tumesitaja kazi, za viongozi, kazi ya Rais imeandikwa kabisa katika Katiba siyo hiyo blanket kwamba there shall be a President. Lakini safari hii tumeandika sasa kazi yake ya kwanza ni hii, kazi yake ya pili ni hii, kazi yake ya tatu ni hii, kazi yake ya nne ni hii, hawezi kufanya hii, hawezi kufanya hii. Kazi ya Waziri Mkuu pia tumeiandika. Na kazi ya Makamu wa Rais pia tumeziandika, sababu saa hii Makamu wa Rais yuko pale tu. Akiambiwa wewe nenda Geneva basi, safari huyo Geneva. Akiambiwa mimi naondoka wewe kaa hapa bwana basi yuko pale pale. Lakini safari hii tumeandika pia hata kama vile bwana Rais yuko lakini makamu wake Rais kazi zake vipi? Tumeziandika.

Tofauti nyingine tumesema Mawaziri hawatakuwa Wabunge, hiyo ni tofauti kubwa. Mawaziri hawatakuwa wabunge au wabunge hawatakuwa mawaziri. Ukiwa wewe Mbunge umbunge tu shugulikia na mambo ya kaloleni, kwa sababu ukiwa mbunge na ukiwa uwaziri kuna habari mbili pale hutokea. Kama kweli wapenda kazi yako basi watu wako wa Constituency watapata shida, hupatikana. Kwa sababu wewe u mbunge wa Kenya nzima kama waziri. Kama waziri wa maji, basi ni maji kutoka Vanga, mpaka Lamu, mpaka Lokichogio, mpaka Kisii maji ni wewe. Haya muda utapata wapi halafu uongelee maji ya Kaloleni? Kwa hivyo ikiwa utafanya kazi ya kitaifa sasa watu wa Kaloleni watapata taabu. Au uamue wewe kwa vile ambavyo umbunge na uwaziri wa maji basi watu wako ndio watafaidika, Kaloleni maji yote ya Kenya nzima yaletwe hapa wale wangine shauri yao. Tumeondo hiyo, tumesema mawaziri watakuwa nje, hata si wabunge kamwe. Professionals – wakati wa maswala bado bwana, mimi naeleza halafu nitawapatia nafasi. Tumesema kwamba mawaziri watatoka nje ya Bunge. Tena tumesema wawe ni professionally qualified, vile vile nilivyosema, Waziri wa Afya awe ni Daktari ambaye amesomea shindano na kupasua na nini, Waziri wa kilimo alisomea Bachelor of Science Agriculture. Hiyo ni tofauti ingine tumesema.

Halafu tumesema kwamba Provincial Administration – Machief, naibu wao kwenda mpaka kwa PC tomeondo. Hiyo ni tofauti kubwa. Tumeondo kwa sababu wananchi walilia na wakasema either hawaoni kazi muhimu za wengine, wengine wakasema kwamba hawa ni wakoloni ni njia moja ya kuendeleza ukoloni mamboleo, visa vingi vikatajwa vyta wananchi kulalamika kwamba wanatezwa sana kwa hivyo kilio chenu tumesikia tumeondo, hiyo ni tofauti kubwa.

Pia tunaondo Administration Polisi. Administration polisi tutawatia kwa polisi hawa wa kawaida. Sababu wale wanatumiwa na Provincial Administration kufanya yale mambo mengine mliyasema kwamba hayafai. Kwa hivyo administration polisi hawako, nafikiri huwa munawaona kwenye road block ambao si traffic polisi lakini kwa sababu ametumwa na yeze apate mfugo ambaye utaenda mahali pengine. Lakini hana haki kulingana na sheria kusimama barabarani lakini wako wanafanya kazi. Kwa hivyo tumesema hizi polisi forces tuifanye iwe polisi force moja kwa sababu wao wenyewe ndio wataamua yule ataenda barabarani yule ataenda kutoa mnazi yule atafanya nini lakini under the polisi force.

Halafu pia tumesema hiyo, hiyo polisi force yenye iwe iko kwenye Katiba sasa. Katiba ya sasa inasema hii Police Force ni under Office of the President. Sasa tumeiweka Constitutional Office, with a tenure of office. Yule mkuu wa Police sasa ana kazi yake maalum tumemwekea ata-serve maximum miaka kumi na yeze kuchaguliwa kwake ni vile vile atapendekezwa tu na Rais lakini kazi yote ni wapi, Bunge, wabunge wakisema huyu hafai.

Pia Prisions, tofauti ingine ni hiyo prisons pia itakuwa hivyo hivyo. Kwanza tumebadilisha jina tunaita Correctional Service warekebishaji wa watu, tabia za watu, badala ya prison maana yake prison hilo nino limetumiwa vibaya ukilitaja kila mtu ashutuka maana yake hali ya huko prison ni ngumu sana. Kwa hivyo hata hiyo tulifanya ni Constitutional office.

Hata majeshi pia tumeyafanya sasa yametengenezwa na Katiba. Mkuu wa Jeshi sasa sehemu yake iko katika Katiba.

Halafu tunesema kwamba katika viongozi wote wa Serikali wa uma wa haya Matume wote mtu ata-serve maximum miaka kumi. Kiongozi yeote wa Uma. Kutoka mbunge mpaka managing director wote wa mashirika miaka yake mwisho ni kumi. Ni mzuri kumi ni mbaya hapo katikati anaweza kutolewa. Lakini hazidishi kumi hata waziri hazidishi kumi, kumi ni kumi tu, kumi, kumi tumekuwa watu wa kumi kumi.

Halafu tofauti ingine tumeangalia upande wa mahakama na mnajua upande wa mahakama ile ambayo kuna kesi tatu, nne sijui. Sisi wenyewe hapa tuna warrant ya sasa lakini tunasema ah, ah. Wacha turekebishe kwanza halafu mtakuja tijiandae. Tumesema kwamba mahakama tumeirekebisha sana, tofauti tumeweka, pia tumeweka Supreme Court ambapo ilikuwa haiko hii. Tumeweka Supreme Court iwe ni court ya mwisho kabisa, ukitoka court of Appeal bado kulikuwa kuna pengo, kumaliza Court of Appeal watu walikuwa bado hawajaridhika lakini hawajui waende wapi. Sasa tumeweka Supreme Court pale juu. Halafu pili tunesema mahakama ziwe zinaenda chini zaidi badala ya kwamba usafiri kilometer 100 kwenda kujibu shtaka sasa tunesema ziwe karibu zaidi na wananchi. Hiyo ni tofauti ingine tunaweka.

Na katika mahakama tukienda kwa Islamu Kadhi's courts, sasa tumezitengeneza vizuri, badala ya Kadhi wawili au watatu, vile walikuwa Kenya nzima, tumewaweka 30 sasa kwa hivyo watakuwa distributed, na tumeweka National Kadhi, Provincial Kadhi, District Kadhi pia tumeweka. Halafu Kadhi hatachaguliwa na Rais, kwa sasa anachaguliwa tu kama civil servant safari hii kutakuwa, itabidi Rais azungumze na Judicial Service Commission halafu na Waislamu wote, je huyu afaa au hafai? Ndio huyo achaguliwe ni Kadhi, hiyo ni tofauti ingine tumeweka.

Halafu tofauti ingine tunesema kwamba nguvu za Serikali ya umoja tumeziondoa; unitary government. Sasa tuna Serikali nyingi sasa wengine wameshaanza kujadili kwamba ingawaje mmetoa ile moja ambayo ilikuwa inafuta zote, lakini sasa hizi zingine ni nyingi sana. Wengine wanasema ndio vizuri hiyo hiyo. Kwa hivyo saa hii tutaanza na village council, vile vijiji vile via wazee vile, hapo kuna Serikali yake. Sasa wenyewe mtaamua wale mtawateuwa tu mzee fulani, mzee fulani, kijana fulani, kijana fulani, au mtafanya uchaguzi Katiba hapo imewapa uhuru. Halafu kutoka pale kuna location. Locational Council Serikali nyingine hiyo, halafu tukitoka hapo kuna ya district. Hiyo ndio Serikali yenyewe kubwa maana yake kwa district pia uwezo wa kutoza kodi pia mnayo pale kwa district sasa. Wananchi watachagua Serikali yao ya wilaya. Halafu tunayo Provincial government, haitoshi bado ili watu wa eneo moja wajue wanatalwa kivipi, halafu ndio tunapatia mwisho kabisa Serikali ile ya Nairobi. Unitary government. Kwa hivyo hiyo ni tofauti kubwa sana ambayo tuko nayo hapa.

Tofauti nyingine ni kwamba na nimeshueleza ingawaje indirectly safari hii tumeweka nafasi nyingi za uongozi. Executive, kuna Rais na Makamu wa Rais, kuna Waziri Mkuu, kuna makamu wawili wa Mawaziri wakuu, halafu kuna Mawaziri wenyewe wa wizara wenyewe wa Wizara ni kumi na watano nimewataja katika Katiba, Ministries ni kumi tano tu. Halafu na mawaziri wenyewe ni kumi na tano. Sio kama sasa wizara ni kumi na tano, lakini mawaziri ni thelathini. Manaibu wa mawaziri ni naibu mmoja kwa kila wizara, moja moja basi. Hakuna haja ya kuweka watu wengi ambaao kazi zao hazijulikani.

Halafu upande wa Ardhi ni tofauti moja kubwa hiyo. Tofauti kubwa kwanza tumesema, wageni ambaao si wananchi wa Kenya, hawatakuwa na ardhi hawataweza kumiliki ardhi. Wao watamilki ardhi kwa kuponyi tu lease tena isizidi miaka 99, hiyo ndio maximum kabisa huyo ameonewa huruma kabisa, 99 kwanza tulikuwa tumesema 40 lakini tukapingwa --- ni 40. Baada ya miaka 99 tena tunaweza tukasema we nenda zako kwenu hii ardhi hii sasa ni yetu. Lakini wana ruhusa ku-own land kabisa haiwezekani sasa, kwa sababu wananchi wengi wa Kenya wamesema wageni wana ekari mia moja, sisi hatuna hata robo. Itawezekana vipi. Tumesikia kilio chenu na tumesema kwamba ardhi itakuwa ni ya wananchi wa Kenya. Pia katika mitindo ya Ardhi sasa tumezibagua zile aina tatu za umilikaji wa ardhi na tumezitaja katika Katiba, zilikuwa haziko, Public land Ardhi ya uma, Private land Ardhi ya watu binafsi, na Community land, ardhi ya wenyiji. Hii ambaye yaitwa Trustland sasa, tumeitoa kule kwa trust, kwa sababu trust land yiko kwenye County Council, lakini anayetoa hiyo ardhi ni Commissioner of Lands. Hawa wa County Council wafanya kuletewa barua tu fulani huyo tumejhampa, acre kumi na hamna la kufanya. Sasa ni yenu tu jina lakini mamlaka yote yako Nairobi. Sasa tumeondo hiyo. Ardhi itakuwa ikipeanwa na wenyiji, kila ardhi ambaao ni Trust land sasa ni ardhi ya wananchi, sasa wananchi wenyewe tunawapa uhuru lile neno wananchi mpaka tulitengeneze liwe ni watu ambaao wanajulikana ni kina nani kama wanachaguana wasema tunaweka kamati ya wazee ni wao wenyewe kama watasema ni kabila lote la kambe ndio wananchi ardhi iwe yaho ni wao wenyewe uhuru ni wa wananchi, hii tukiiza ardhi hii haitakuwa ikitolewa kutoka Nairobi. Hiyo ni tofauti ingine kubwa sana. Halafu badala ya Commission of Lands tumeweka Tume permanent, National Land Commission, Tume ya Ardhi, na hii Tume ya ardhi itakuwa na branches katika kila wilaya, matatizo yaende pale lakini sio kuweka mtu mmoja Nairobi Titles Deeds zote zatoka Nairobi, ukiwa na matatizo yeyote, Title zatoka Nairobi mtu apewa Title kabla hajaona pia ile ardhi yake, yuacha akakwambia hii yangu toka. Hiyo tumeondo. Kwa hivyo kwa ufupi tofauti kwamba zilizoka katika hii Katiba ya sasa na ile Katiba itakayokuja ndio hizo.

Sasa tukienda kwa Katiba yenyewe, details zenyewe, wale ambaao mko nazo nafikiri mmeona pale. Tumeweka, ingawaje kila mtu ana pahali pake ambapo yu apapenda sana lakini sisi tunasema Katiba ni kila kitu.

Kwanza tumesema katika kifungo cha kwanza hizo nakala tunataka kuzitumia kesho kwa hivyo mtatusamehea kidogo – Katika kifungo cha kwanza Chapter One Sura ya kwanza hapa sana tunazungumzia kuhusu umuhimu na uwezo wa wananchi wa Kenya. Katika maisha ya Katiba. Hapo ndio tunazungumzia Supremacy of the people. Wananchi wenyewe ndio wametengeneza Katiba, kwa hivyo tunaandika pale pia wananchi wenyewe ndio wanaweza kuibadilisha Katiba. Kuna mambo fulani ambayo wabunge wanaweza wakabadilisha lakini kuna mambo muhimu ya kuhusu Katiba hawaguzi bila ya wananchi. Hiyo tumeeleza katika kifungo cha kwanza kwa sababu mlilalamika kwamba kurekebisha Katiba inachukua dakika kumi tu

Bunge wameshapitisha. Katiba hiyo wanarekebisha wenyewe mwaletewa nyinyi, sasa tumesema hapa wananchi wenyewe ndio ambao wana haki ya kutengeneza kuilinda na kuibadilisha Katiba. Si ruhusa kabisa, kwa wabunge kufanya hivyo bila ya wananchi. Halafu Katiba tumeeleza bado ni kwamba ndio chombo kikubwa cha sheria katika Kenya hii. Hicho ni kifungo cha kwanza.

Kifungo cha pili, sura ya pili na kuna details hapo mtaangalia kama mna maswali tutazizungumza. Tumeeleza the Republic, yaani taifa letu ni lipi, kwa sababu mlisema kwamba Katiba yetu haina reference ya taifa, inaanzia tu, There shall be a Republic, basi nafikiri hiyo ndio sentence ya kwanza katika Katiba ya sasa ya Kenya: There shall be a republic ... Halitaji ni lipi hilo republic, inaambiwa tu, Tutakuwa na taifa. Sasa tumesema taifa letu tutaliandika kabisa. Kwa hivyo tumetaja kwamba Kenya ni nchi huru na halafu tukaandika eneo ambalo ni la Kenya, ile Ardhi ambayo ni ya Kenya, pia tumeandika. Ukiangalia mwisho kule nyuma kuna schedule, first schedule, Territory of the Republic of Kenya. Eneo ukiangalia hapo tumeandika, wale ambao wamefanya Geographia, au Survey tumeandika kwa alama zile za beacons. Kuanzia Lake Victoria katikati mpaka Lodwar mpaka wapi, yaani ukifwata hizo beacons, kama waenda na kalamu hivi utaenda uchore, uchore, ukimaliza umepata Kenya. Hiyo ndio ardhi ya Kenya. Kwa sababu hiyo mtu yejote akichukuwa futi moja tu ya Kenya sisi tuko tayari kwenda vita, sababu sasa tumeieleza, tumeuchora ule mpaka katika Katiba. Zamani ilikuwa hakuna. Na ni kwa sababu ya wakati lakini tunatengeneza hata ramani, map ya Kenya ile finally ikitoka itakuwa na ramani ya Kenya kuondoa mzozo kabisa.

Na bado tunasema Nairobi itakuwa ni Captial City. Lakini ikiwa kuna haja ya kuondoa vyombo fulani vya Serikali kwenda miji mingine tumesema inawezekana. Kama, tunatoa mfano wa South Africa, wametawanya Bunge liko Cape Town. Judiciary iko Johannesburg, Executive iko Pretoria; tofauti, tofauti sio vitu vyote vinaenda pahali pamoja. Hilo pia tumesema. Kigungu number nane, kimesema sheria inaweza ikapitishwa namna hiyo.

Halafu tunasema pia Lughu: Tumesema official languages zile lughu ambazo ni za rasmi ni Kiswahili na Kingereza lakini lughu ya taifa tumekubali ni Kiswahili kwa hivyo ukienda pahali popote ukisema Kiswahili sio hatia sasa. Na tumesema katika kifungo number 9(3) tumesema kwamba ni lazima wafanye sheria ipitishwe kuhakikisha kwamba Swahili inaingia katika lughu ya Serikali.

Katika Sura hiyo ya pili, pale mwisho kifungo cha 13 tumeeleza tumependekeza sikukuu za kitaifa. Watu wengine walilalamika wakasema ni nyingi sana, wengine wakasema hazitoshi, wengine wakasema kuna nyingine zimesahaulika, kwa mfano Mau Mau walisema wanataka Mau Mau day, walipigania uhuru, wengine wakasema wanataka Heroes day wengine wakasema mambo mengi. Tumesema tunapendeza Madaraka Day, tarehe moja iendelee kuwa sikukuu ya kitaifa. Halafu tarehe 12 siku ya Jamhuri Day tumependekeza iwe ni siku ya kitaifa. Halafu hii nyingine, hatkuandika tarehe pale, lakini ni siku ya Katiba, siku ile Katiba itapitishwa Bunge pia nayo iwe ni siku ya kitaifa kwa sababu maana yake ni kama tumejikomboa. Kwa sababu hiyo tumeondoa Kenyatta Day, tunaondoa Moi Day, sijui nani Day. Hizo zote tunazitoa.

Halafu sura ya tatu – National goals values and principles. Haya ni maadili ya ambao kila mwananchi wa Kenya atatakiwa kuayazingatia. Halafu pia tunaeleza duties of a citizen, majukumu ya mwananchi ni nini, siyo kusema tu serikali, serikali yatufanyie, wewe mwananchi nawe pia uwe na jukumu lako. Kwa hivyo tunaeleza pale katika kifungo cha 15 mwananchi ni lazima alinde Katiba yake. Lazima awe anafanya mambo ya demokrasia, lazima awe ni mtu wa kufanya kazi sio mtu wa kukaa tu hivi kusurura ovyo tumeeleza pale. Ni lazima awe anahuksika katika maendeleo. Na lazima awe anafwata sheria. Tumesema majukumu ya wananchi pale.

Katika kifungu cha 4 ni citizenship. Nafikiri nimeeleza pale mwanzo. Kulikuwa na shida nyingi sana wananchi wengi wakieleza habari ya watoto ambao wamepatikana hawajulikani kwao ni wapi, wale tumewapatia nafasi pia kwamba wawe ni wananchi wa Kenya. Halafu tunesema kuna sababu nyingi tumeangalia za watu ambao wanataka kuwa na citizenship mara mbili yaani uraia wa Kenya tena pia ni raia wa Uganda. Sababu ambazo zilikuwa ni nzuri ni nyingi zaidi kuliko zile ambazo ni mbaya. Kwa hivyo ambaye anataka anaweza lakini tumeweka vikwazo pia ambacho kitamunyima automatically uraia wa Kenya mtu kama atakuwa na raia ingine lakini afanya mambo fulani kule. Tumeyataja pia hayo.

Halafu Bill of Rights – Kifungu cha tano, sura ya 5, Bill of Rights, zile haki ambazo nimesema hapa ni ndeu sana kuna haki nyingi hapa, tumetoa tunasema kwamba freedoms. The State shall observe and respect, Serikali itakuwa na lazima inalazimishwa kuakikisha, tunasema kwamba ni wajibu sasa, sio kwamba ni privilege, tunasema sasa ni wajibu wa Serikali, ni wajibu wa taifa kuwapatia wananchi haki hizi tuliyotaja hapa. Sio privilege tena, sasa hii ni lazima. Ni wajibu, lazima Serikali ifanye mambo haya yaliyoteuliwa hapa na ipitishe sheria ya kuhakikisha kwamba tunayafwata.

Haki za kimsingi kwa mfano tunasema kila mtu ako na haki ya kuishi kwa hivyo hiyo sheria ya kunyonga wafungwa tunaiondoa maana yake tunakuta kama maisha ya binadamu ni, afadhali kumufunga milele, maana yake ukimfunga milele aishi tu lakini hana raha kama mimi niko huru.

Halafu sheria tunesema kwamba hakuna haja wananchi wa Kenya kubaguana either kwa dini kwa lugha, kwa mila kwa kabila, kwa eneo kwa rangi kila aina ya kitu, tunasema wananchi wa Kenya wako sawa. Sote tuko sawa kama wananchi wa Kenya.

Halafu tumetoa pale haki za akina mama, tumetoa pia haki za wazee kwa sababu wazee tunesikia wakilalamika mzee wangu hapa, wazee wanalamika kwamba kazi yao kuitwa kama mambo yameharibika tu, ndio wanaambiwa iteeni wazee lakini mambo kama yaenda vizuri wazee wanashida, na walikula miaka yao. Sasa tunesema wazee pia should be free from all forms of discrimination. Wasibakuliwe wala wasifanyishwe kazi sana wala wasitumike kupita kiwango kwa sababu wao ni wazee.

Watoto haki zao tunesifuatisha kama ilivyopitishwa ile sheria ule msaada wa watoto, kuzipunguza bado tumejua kwa family iwe bado ndio unity. Tumeangalia haki za wale ambao wasiojiweza. Tumeangalia pia haki za security. Freedom and security mtu awe na uhuru wa kutembea pahali popote. Tumesama kazi zozote au tabia za utumwa tumeziondoa.

Freedom of expression kila mtu ana uhuru wa kujieleza bora asitukane. Freedome of religion kila mtu ana haki ya kufanya au kuendesha mambo yake ya dini isipokuwa tumetoa vikwazo kwa wale ambao walikuwa wanasema kuna dini zingine zinapigia watu kelele usiku mzima. Kesha sijui nini hizo. Tumesikia vikwazo hapa lakini kila mtu ana uhuru wa kuabudu dini yake na asifanyishwe kazi siku ambayo dini yake haimuruhusu. Kwa sababu tulikuwa na watu wa Sabato walikuwa wakilalamika tunesema ah, ah, kama mtu yu wafanya kazi kilindini lakini mtu wa Sabato msimupange shift ya Jumamosi. Msipange kabisa na kama ni Muislamu anatakwa kwenda Ijuma mwenyewe akapumzike haya. Time zake za swala zikifika mwacheni aende. Lakini watu wote wawe wanaweza kufanya mambo yao wanavyotaka.

Halafu kuna access to information – haki ya kupata habari haswa za Serikali. Tumesema kwamba (**end side A tape 1**)

Haya si mambo yenu haja yenu kukula nyinyi haya. Sasa kuna haki kwamba habari zozote za mwananchi za serikali mwananchi ana haki ya kwenda ku-demand haswa mimi nataka copy fulani ya haya mambo. Hiyo ni tofauti kubwa sana.

Freedom of association, unaweza kujiunga na mtu yejote, au kushikana na mtu yejote kufanya mikutano halafu na political right yako unaweza kuendesha kwa vyovoyote na kadhalika. Hizo ni nyingi kama ningesema hizo ni nyingi sana hizo na mtasifikia na mtaona ubaya wake na uzuri wake. Kwa mfano ukiangalia section 70 kifungu number 70 – wale ambao wameshikwa na askari wanangojea mahakama, wanangojea kesi wako rumande pale. Walikuwa watu ambao wamedhulumiwa sana. Saa hii tukishikwa, nimushukiwa, heri afadhali yule ambaye alihukumiwa akapelekwa ndani, maana yake mambo yake yashajulikana huyu aliua basi lakini huya amba ni mushukiwa, pengine hata masikini huna hatia utapta taabu sana, kitambo wakupeleke kortini wewe watakiwa kukubali kila kitu tayari maana yake vile ulivyo fanywa kule hutaki tena kurudi kule. Sasa tunesema, mtu anayeshikwa mushukiwa bado ana haki zake kama yule yuko nje. Bado ana haki zake mpaka awe approve kwamb huyu ni kweli amefanya jambo hili na jambo lile. Kwa hivyo yeye hafurusiwe kutukanwa, wala kupigwa na akienda ndani katika kifungu kile cha 73 pale number 2 (b) akifichwa ndina apatiwe vifaa vyote accomodation facilities, nguo nzuri, pahali pa kulala pazuri, chakula kizuri, madawa kama ni mgonjwa nakadhalika. Tumeeleza. Hiyo ni tofauti kubwa sana tunesema. Na ikiwa serikali imesema haina dawa aruhusiwe kumwita daktari wake ache amutibu pale, ikiwa serikali itasema sisi hatuna dawa. Anaruhusiwa kuita dakitari wake pale, kama ni mtu wa kuswali atakikana apatiwe mahali aende akaombe mungu kama ilipo nje kama ni mtu wa kusoma mwenyewe hukuwa na course yake yuwa wafanya serikali yatakitana immuendeleze. Maana yake hana hatia bado, hajaamliwa kwamba ni kweli ama uwongo. Kwa hivyo huwezi kumharibia maisha yake wakati yuko pale. Hiyo ni tofauti kubwa sana ambao wananchi walikuwa wakielezea na mambo mengi ambayo tunayaelezwa katia kifungu hiki. Hiyo ni sehemu ambayo watu wengi walisema sana. Ndio maana iko na kurasa nyingi sana. Ndio sababu madhambi mengi wananchi walikuwa wakisema yako katika area hiyo.

Haya twende upande wa Uchaguzi. Tumesema kwamba uchaguzi utakuwa ni wa secret ballot. Kura ni ya siri uchaguzi wa aina yejote, mambo ya mikono mambo ya nini hiyo tumeondoa sababu kura ni siri yako na haswa kwa ungozi ambao tunataka sasa

ya kwamba kuna viongozi ya Village, kuna viongozi location, kuna viongozi district kuna viongozi province. Tukisema kwama ni kwa mkono, mimi nikijua kwamba yule hakunijakuwa na sasa mimi ndio kiongozi, basi patakuwa na shida. Na tumeondoa Provincial Administration chief atakuwa hayuko sasa kuna mambo pale yafanyike, na kama unajua kwamba yule hakunifanya, hakunipigia, sasa kutakwa na vita kwa hivyo afadhali iwe ni ya siri. Tumesema kura zote ni za siri.

Halafu tumesema kwamba kila mwananchi ana haki ya kupiga kura. Umri tumeweka ule ule, miaka 18. Halafu tumesema kura ziandikishwe throughout, siyo kungojea mwaka wa kura ndio uwende ukajukuwe, tumesema they should be continuous, registration of voters. Iwe inaendelea kila siku.

Halafu tumesema pia kura zitahebiwa kwenye kituo. Ukiangalia katika kifungu cha 81 tumesema kwamba kura sitahesabiwa pale pale basi kama ni wizi kama ni nini utokea hapa hapo. Mambo ya kusafirisha madebe siju tatu siku nne hiyo tumeondoa, wananchi watahesabiwa pale pale waambibiwa katika kutuo hiki fulani ndio ameshinda. Sasa twende kule kwengine (clapping of hands). Na pia tumesama lile debe lile litakuwa transparent waliona lile limejaa. Transparent boxes katika kifungu tumesema the ballot boxes to be transparent. Habari ya kuleta lile jeuzi lile halafu halina kitu lakini mtu aliunua, ah, haifai. Kwa hivyo itakuwa transparent na tutahesabu hata hapa tukiondoka hapa twajua fulani ameshinda kituo hicho.

Halafu tena tumeunda upia Tume ya uchaguzi. Tumepunguza ile hesabu ya wale watu Makamishna wale wa kwenye Tume. Wasizidi kumi na tumesema mmoja atoke kila mkoa. Badala ya sasa ni 22, 23 tumesema wawe maximum kumi tu na sasa pia wata-serve kwa miaka kumi. Na Tume hii tumeipa kazi ingine sasa kazi yake itakuwa ni kuhakikisha kwamba wananchi wanaandikishwa wanapewa vikadi vya kura kila siku. Halafu pia hawa watashirikiana na Tume ingine ambayo tumeiunda ya Boundary Commission, mipaka ya kuangalia mipaka ya Constituencies . Hawa watakuwa wanashirikiana na wale kuangalia mipaka halafu hawa ndio wafanya mambo yote ya kura. Halafu hawa pia wata-supervise political parties. Kwa sababu hii itachakuliwa na wananchi na Bunge ndio litapitisha. Kwa hivyo haiwezi kuwa ni ya chama kimoja. Itakuwa ni ya watu wote. Kwa hivyo itakuwa ni independent Commission. Kazi yake itakuwa ni kuangalia vyama vya siasa na management ya political parties halafu hawa pia watakuwa wanafanya civic education. Bado hii Tume ya kura itakuwa kazi yake nikueleza wananchi kwamba umuhimu wa kupiga kura ni nini maana ya kura ni nini, maendeleo ni nini. Hiyo sasa ni kazi yao ambao zamani ikikuwa hawana.

Halafu tumesema hiyo Tume itaangalia mipaka. Kushikana na ile Tume ingine, lakini hii mipaka tumesema haiweze kubadilishwa mpaka baada ya miaka kumi habari ya kupatiana constituency kwa sababu fulani anaonekana angekuwa ni mtu mzuri kwa hivyo tusimtoe lakini tumwekee yake tumkatie kipande hiyo tumeondoa.

Nimesema habari ya vyama vya kisiasi, vitakuwa registered na Electoral Commssion, lakini kama kun shida ye yote kuhusu vyama vya kisiasi High court ndio itaamua. Na hatukuweka ile number mlikuwa munataka wananchi walisema kwamba tunataka number ya vyama vya kisiasi viwe baina ya vitatu na vitano visizidi hapo, lakini tumesama vitakufa vyenyewe kulingana

na hii taratibu tumeweka hapo maana yake kila chama cha kisiasa ni lazima kiwe, I mean hakuna chama ambacho kitaandikishwa ikiwa kinazingatia mipango ya kidini, vyama vya dini hazitakuweko. Vyama vya kisiasa lakini vya dini fulani, havitaruhusiwa. Luga fulani, pengine waadiko pekee yao hawa havataruhuziwa au racial rangi watu waupe pekee yao waanze chao hakitaruhusiwa au cha kabilia fulani au cha wanawake tu Women's political party of Kenya hicho hakitaruhusiwa namna hiyo. Au cha mkoa fulani pekee yake, regional basis hivyo vyama havitaruhusiwa mpaka viwe ni vya watu wote. Ndio mna chama chenu lakini kina watu wote weupe, wauzi, wekundu, warefu, wafupi, wajaluo, wakikuyu, mijikenda, kila mtu huko pale, basi kitapata registration. Kwa hivyo zile zingine arobaini na ngapi zenyewe tu zitaingia gizani hivi hivi maana yake vingine havina masharti haya.

Halafu tunaenda kwa upande wa Bunge, nimesahau kutaja sas ile tofauti tumeweka sasa tuna mabunge mawili. Kuna Upper House na Lower House. Kinyume na hayo kuna wale wabunge 222 tumeweke Bunge nyumba mbili kama wakati ule wa 1963/64. Wale wabunge mia mbili na kumi watachaguliwa kama hivi sasa, halafu tutakuwa na wale 90 ambao tutawachagua kwa mixed proportion, halafu tutakuwa na wabunge 100 wa Upper House. Sasa haya mabunge mawili yakikutana Lower House na Upper House, ile Upper House tunaita National Council, Lower House tunaita National Assembly, wakichanganyikana ni Parliament hiyo. Hawa ndio ambao tutawapatia kazi za kuangalia checks and balances, Nyumba moja haiwezi kuitisha Mswada ukapita hivi bila ya nyingine kukubali. Na katika hawa wabunge 100 wa ile Upper House 30 ni kina mama. 70 wanaweza kuwa hata kina mama wako lakini wale 70 kila mmoja anatoka kila district. District za Kenya ni 70 kwa hivyo kila district itachagua Mbunge wao moja ambaye atakwenda kwa Upper House, halafu wale 30 ni wanawake kina mama ambapo kila mkoa utachagua 4 mikoa saba, hao ni 28 halafu Nairobi itachagua 2 watakuw 30. Hao ni mia hao ndi wa National Council

Halafu tumesema kwamba qualification wale wabunge wa National Council Upper House, watakuwa na saidi ya miaka 35. Kule ni kwa wazee. Hawa wabunge wengine miaka 21 lakini ile National Council miaka ni 35 kwa sababu wale wanaangalia hawa 210 hawa. Sana kazi yao ni kuangalia wasifanye excesses. Kwa hivyo kwatakikana watu kidogo ambao wamekoma kiumri kidogo. Lakini tumesema mwisho ni miaka 70. Mbunge ye yeyote mwisho ni miaka 70. Hakuna mbunge ambaye atazidi miaka 70, kwa hivyo wale wazee wangu ambao wana tamaa, kama una tama kidogo utatuwia radhi.

Halafu kiwango cha elimu tumeweka ni Form Four, lakini Four four yenye pass. Tumeandika hapa Form Four with a pass siyo kwamba ukakaye darazani nayo siku ya mtihani usifanye mtiayani mana yake hata ukienda ukikaa utapata zero zote lakini utapata certificate. Kwamba wewe ni Form Four bado, hujakuwa Four Four mpaka tutaangalia ulipata ngapi katika Hesabu, English kwa hivyo hata Division Four pia uko na shida. Hawa watu wa D+ mko na taabu. Baada ya kusema graduate watu wengi walisema kwingine hakuna wa-graduate wazuri wengine wakasema uongozi watoka kwa Mungu siyo lazima uwe umesoma, mana yake kuna watu walisoma na bado hawafai kabisa na ni viongozi, sasa tumekuwa liberal hapo tumeweka katikati.

Na wabunge mwisho wao hata wao ni miaka kumi hata kama ni mzuri vipi ukimaliza miaka kumi nyumbani.

Halafu muna ruhusa vile nilisema ya kumtoa mbunge ambaye hafanyi kazi. Na tumeeleza ni vitu gani amba o vyaonyesha kwamba ni ishara gani kwamba mbunge ule hafanyi kazi kwa hivyo mkiziona hivyo mtajua mtafanya nini, petition itaenda kwa Speaker halafu uchaguzi utafanywa tena. Haya yote ni mambo ya wabunge.

Halafu tumeeleza kwa sababu bunge huwa linakosa quorum, saa yote tunasikia bunge limekosa quorum. Tumesema kazi yao ni full time. Kazi yao ni full time ili wazikoze kule bunge na tunesema quorum itakuwa ni 30% badala ya 20% hivi. Sasa ni 30% sasa itawalazimu na kukosa kuhudhuria bunge ni sehemu moja, ni ishara moja kwamba mbunge hafanyi kazi imeandikwa pale kwa hivyo mkisikia mbunge wenu hajaonekana wala hajasema bunge wiki 3 sasa mwanze kufanya wasi wasi maana yake hiyo tayari ni moja ithini sehemu, mkimfwatilia sana hapo mtamtoa, sasa itawabidi lazima wawe hapo, lazima wachangie, sio kwenda kulala.,

Halafu tunasema katika Bunge, saa hizi sheria wabunge watajadiliana wapitishe mswada halafu itatakikana uwende kupitishwa na Rais. Lakini haitowi muda Rais anaweza kukaa nayo miaka mitatu miaka minne, nyinyi mwatia fujo hapa yeye anakaa nayo. Sasa tumempa muda katika wiki mbili ukiletewa Mswada ni lazima utiye sign. Isizidi mwesi moja lazima utiye sign. Kama hataki atamwambia Waziri Mkuu, naye ataleta tena mjadala Bungeni uzungumziwe kikao kingine basi baada ya wiki moja. Ile round ya pili ikifika sheria yenye we ikubali wiki moja tu badala ya kuwekwa miaka, miaka, hii haitakikani.

Halafu Bunge litakuwa na ratiba yake siyo kwamba mtu afikirie tu hawa ngoja niwapeleke nyumbani au saa hii kuna mjadala hot, kwa hivyo Bunge lafungwa tuwambiwe endeni nyumbani mieze miwili. Wamekuja jusi na warudishwa tena nyumbani. Itakuwa na Timetable katika kila mwakwa tunajua Wabunge safari hii watakaa tarehe moja mpaka tarehe tano. Tarehe tano mpaka, kila mtu awe ajua.

Na tarehe ya uchaguzi nimesahau kueleza, tarehe ya uchaguzi pia itakuwa, tumependekeza mweze wa nane kila mwaka kasoro mwaka huu. Lakini tumependekeza mwezi wa nane Jumanne ya kwanza ya mwezi wa nane. Iwe ya julikana siyo kila mtu awe ameweka ni siri halafu watu wana-guess ni siku gani.

Haya twende kwa ungozi Rais. Nimeeleza powers zake nimeeleza kazi zake ni nini nimeeleza pale. Kwa kweli tumetoa zile powers nyingiza Raisa ambazo watu, wananchi walikuwa wakilalamikia tumeziondoa, kama nilivyo eleza pale mwanzo Rais hawezি kufanya kitu, hawezى kabisa hakuna kitu cha kufanya hapa isipokuwa kumuuliza Waziri Mkuu kuna sheria fulani ilipitishwa juzi bungeni, hebu nielezee. Hiyo hawezى kushauri mtu. Lakini haya maneno mengine yote hawezى. Mpaka aende Bunge. Akitaka kuteuwa mtu mpaka aende Bunge, akitaka kufuta mtu mpaka aende Bunge. Akitaka kutengeneza kitu mpaka aende Bunge. Yaani sasa kazi zake lazima ashauriane. Hakuna mtu ambaye ni mtawala wa nchi awe ana-run hiyo show peke yake. Tumehakikisha Hiyo. Hata Waziri Mkuu ni lazima awe anashauriana na wananchi na watu wengine.

Halafu tunaenda upande wa Rais anaweza kushtakiwa hiyo haimo katika Katiba ya sasa. Lakini sisi tumeeleza tunapendekeza maana yake nyinyi mlisema na tumeandika hivi, Rais kama afanya makosa afanya madhambi wizi au nini. Huyo tutamshtaki tumtoe na akitoka pale aingia kortini tena kujibu mashtaka.

Sehemu zingine zimeeleza nani atajukuwa baada ya Rais kama ni mgonjwa, huyuko hizo ni details ambazo mpaka sasa ziko. Halafu kama nimesema tutakuwa na Waziri Mkuu na manaibu wawili. Waziri mkuu ni yule ambaye atachaguliwa kutoka kile chama ambacho kitakuwa na kura nyingi zaidi katika bunge.

Hawa mawaziri nimesema kwamba hawatakuwa wabunge lakini wana haki ya kuitwa kwenda kueleza wabunge wamefanya nini katika wizara zao kwa hivyo watakuwa wakifika kwa Bunge kueleza kama wataitwa lakini otherwise wao si wabunge.

Halafu upande wa mahakama nimeeleza sijui kwamba tulikuwa tumezuiwa tuiseme. Lakini tunaendelea hivyo hivyo. Mahakama mnajua vile mlivyosema zina shida mbili sana, corruption halafu muda mrefu kesi yaweza kukaa hata miaka kumi, wapelekwa huku tu ikifika mention leo ikifika yatajwa tena mwezi wa January ukifika wapewa tarehe ya mwezi wa saba mwaka ujao, ikifika tarehe ya mwezi wa saba mwaka ujao, ikifika mwezi wa saba, mwezi wa January namna hiyo tu haijulikani, tumeweka muda sasa kesi ni lazima isikiliswa katika miaka miwili na iishe. Kam hayawezekani basi mambo mengine. Lakini kesi ina muda hakuna kesi isiyoisha. Lazima tuweke muda tumeweka hivyo katika Judicial system.

Halafu mawakili na ndio vita ambavyo wamekuja navyo hivyo tumesema hawa wata-retire kwa miaka 65. Kuna story ya majaji hawa. Saa hizi wana-retire na miaka 74. Lakini malalamiko tuko nayo wananchi ni kwamba huwa kidogo wale wazee wewe unaeleza kitu yako yeze analala. Wengine wamesema hivyo, na uchovu mwingi, wamefanya kazi miaka mingi basi tunaona hawa ni senior citizens wacha wapumzike lakini kama atafanya kazi sana ni miaka 65. Halafu wale majaji wa high court na Supreme Court wale hawachaguliwi na Rais tena, wanachaguliwa na Bunge. Bunge ndio lina haki ya kuwachaguwa maana yake inaonekana ukichakuliwa na mtu moja au Waziri mkuu akiwachaguwa watakuwa wanasikiliza kesi lakini lazima waulize kule. Sasa huyu tumfunge au tusimfunge? Wakiambiwa mfungeni hata kama hakufanya kosa atafungwa. Sasa tumesema Majaji watachaguliwa na wabunge.

Halafu tumechagua Judicial Service Commission ambao itakuwa na watu wengi sana watu 21 nafikiri. Na ina kila sehemu ya Kenya ya wananchi wako pale. Judicial Service Commission. Hawa Judicial Service Commission., ndio watachagua majaji kina nani, makadhi kina nani. Na kama kuna mtu anataka kupelekwa Supreme Court hawa ndio watapendekeza. Kwa hivyo ni kundi kubwa sana. Kuna mkuu wa sheria pale, kuna mwanamke wa kiislamu pale, kuna Supreme Court Judge, kuna majaji karibu watano pale, Chief Kadhi, kuna mawakili wawili kuna walimu wa Chuo Kikuu ambayo ni walimu was sheria. Kuna watu wengi pale kuna Chairman wa Public Service Commission. Halafu kun watu watatu wakawaida kutoka kwa NGOs. Watu tu wakawaida wafanyi kazi wa NGOs, nao wataingia kwenye, ili ku-represent masilahi ya wananchi.

Halafu tunaenda kwa Serikali za mitaa. Serikali zile ambazo tumesema tunaondoa serikali ya --- nguvu zake tumezipeleka kwenye serikali ya kijiji, serikali ya location, serikali ya district na serikali ya Mkoa au ya Jimbo. Zote nizieleza wenyewe watakuwa ni kina nani, uchaguzi utafanyiwa viyi tumeelza pale.

Halafu tumeenda upande wa Ardhi. Na kama vile nilivyo eleza ardhi sasa itakuwa ni ya wanachi wageni hawatakuwa na ardhi na tumeunda National Land Commission inaeleza zile aina tatu za kumilki ardhi tumeondo trust land tumeweka kwa wananchi. Halafu tumeeleza pale kwamba ingawaje haikodirect lakini tumeeleza kwamba ikiwa uko na ardhi yako halafu ukundue dhahabu, dhahabu ni yako, au ukundue mafuta, mafuta ni yako sio kwamba siyo kwamba uje utolewe pale maana yake pamepatika mafuta uambiwe siyo yako tena hii. Maana yake wewe hukujua kwamba pale pana dhahabu sasa sithani vile kwamba hukujua.

Masingira, Katiba ya sasa haina mambo ya masingira kabisa kwa hivyo hii ni section ambayo imelete mambo mengi ya protection ni sheria sasa ni lazima wananchi wa Kenya wote wawe wanalinda masingira. Natural environment, wanyama, miti mbuga za wanyama zile na tumeunda Commission inaitwa National Environment Management Commission, kazi yake ni kuangali momonyoko wa ardhi na kadhalika.

Halafu pesa za uma – Public finance, kuna shida kubwa sana hapo. Nafikiri corruption imeingia hapo na uchumi wetu umesorota sababu ya hizi pesa za uma mabilioni na mabilioni yanapotea. Sasa tumefunga funga nut pale kidogo. Kwanza hakuna mtu hakuna mtu anaweza kuwatoza kodi bila ya kwamba imepitishwa na Bunge. Hakuna, si ruhusa kabisa kwamba mtu acae tu aseme sasa shilingi tatu tatu za kila kilo ya korochi zile zinaenda kulipwa nani. Shilingi mbili mbili sijui katika kila kilo ya nazi sijui zaenda kwa nani. Hiyo imefutwa mpaka tukubaliane katika bunge kwanza.

Halafu kun ule mfuko wa kitaifa – Consolidated fund. Huu mfuko wa kitaifa una changiwa na watu haina nyingi tumewataja pale, na pesa kutoka kwa ule mfuko wa kitaifa tumeeleza sasa kinaganaga nani atazitoa pale. Halafu wakati wa kutengeneza Budget tunaeleza kwamba budget itatolewa kama miezi miwili kabla wananchi kwanza kujadiliana. Siku hiyo ya budget ni siku ambaye watu wamekubaliana. Saa hizi huwa ni siri mpaka Waziri wa Fedha anaingia pale na briefcase yake ndio muambiwe kwamba sigara zimeongezwa bei, maziwa yameongezwa bei. Tunasema itakuwa sasa imeshatajwa kitambo mwezi miwili kama hivi sasa tuje tukae. Yeye twataka kuongeza bei ya pombe mwasesmaje? Wakajadiliane bei ya mkate twataka kuongeza mwasesmaje? Tujadiliane sasa ikifika ile siku ya Waziri kusema ni kama kitu ambacho watu washajua kwamba mwaka huu tutapata kitu fulani kuliko kufanywa kama ni siri. Na hiyo kutengeza budget tumeweka mtu pale Controller of Budget. Yule Controller na Auditor General tumewakata mara mbili tumewagawanya watu wawili sasa huyu mmoja kazi yake ni madiriyu na huyu mwininge ni kuangalia matumishi.

Na hapo wananchi walilalamika kuhusu pesa kwamba pesa zetu zisiwe na picha ya kiongozi alioko. Tumekubali., Kwa hivyo

pesa itakuwa either ina Mt. Kenya au Lake Victoria au Twiga au simba, lakini si mtu yule anayetawala. Kwa sababu tukisema Rais awe anatawala miaka kumi katika miaka arobaini tutakuwa na viongozi wanne ambao wame-retire, sasa itakuwa kila miaka kumi sarafu yetu yabadilika haifai. Kwa hivyo tumeondoa pitcha za Rais katika sarafu yetu.

Public Service Commission, ile Tume yiko katika Katiba na tumeieleza kazi zake watakaoteuliwa pale ni kina nani. Halafu kama nilivyo sema tumeweka Kenya Police Service kwa sababu ile Police Force, lile neno force pia tumelitoa. Wananchi wanasema wale wanatumia lile neno ni wale wenyewe. Huwa ni force na ni force kweli. Sasa tumaita Service angalau wata --- maana yake ni watumishi hawa, siyo walazimishaji, ni watumishi wa uma inaitwa Kenya Police Service.

Halafu na ile Kenya Correctional Services, saa hii inaitwa Prisons, halafu pia, kati majeshi, Navy, Army, Airforce, Defense Forces hizo tumeziweka ziwe kwenye Katiba saa hizi. Halafu kuna Tume, kuna Council, Tume ya Security ya Taifa ambayo itakuwa na Rais wale Makamanda wa Majeshi nakadhalika pale. Hawa ndio wanaweza kupendekeza kwamba Kenya iende kwenye vita halafu wapeleke Bunge.

Halafu kitengo cha 16 tumeeleza leadership and integrity, kiongozi awe viperi halafu sifa ya viongozi tumetoa zile Ethics Code. Kwamba kiongozi hawezu kufanya hivi, akionekana hivi atolewe na kadhalika.

Halafu tena Tume za Kitaifa tumeziweka pale, tumeeleza ni kina nani wanaweza kuchaguliwa kwenye Tume, wata-serve miaka kumi kama wamepata bahati na watatolewa viperi, kazi zao ni zipi, mshahara wao ni kama kawaida itaangaliwa na Tume ya Mishahara na watu hawa watatoka kila katika kila mkoa. Hakuna Tume ambayo itachaguliwa ya watu wa mikoa fulani peke yao watatoka kila mahali. Kwa hivyo tumetoa Tume nyingi pale kuna Commission ya Human Rights and Administrative of Justice hiyo ndio Tume kubwa kabisa. Hiyo ndio ina yule mtu tunamwita Ombudsman. Watu walikuwa wakiteta wakisema wanataka pahali ambapo wanaweza kwenda kuishtaki Serikali, au kushtaki mfanyi kazi wa Serikali. Na achukuliwe hatua badala ya kumpeleka Police kwa sababu polisi ni sehemu yao. Huyo polisi akufanyie madhambi halafu umshitaki polisi station hapo hapo? Utapelekwa hivi, upelekwe hivi utaambiwa we nenda zako bwana tutaangalia. Halafu njoo tarehe 15, sasa tumeondoa ile tumetafuta Tume maalum, ambapo ukimwona askari akutendea madhambi unaenda kule. Na tumesema katika Code of Ethics ni lazima wawe nayo number yao waweke hapa. Hawezi askali kukushika bila ile number. Hata kama ni plain cloth lazima akuonyeshe mimi ni fulani kitambulisho changu hicho andika. Unaweza kwenda kumshtaki yule kwa Tume akaitwa akafanyiwa kesi na akaadhibiwa.

Halafu tunaeleza habari ya kurekebisha Katiba. Kuna vitu ambavyo tumeeleza pale, haviwezi kurekebishiwa mpaka tuwe na kura ya maoni wananchi kwa mfano hatuwezi kurekebisha katiba inayopuzu neno lolote kuhusu ardhi ya Kenya bila ya kwenda kwenye wananchi yaani eneo ya Kenya mipaka ya Kenya mpaka wananchi wakubali.

Uhuru wa wananchi paka wenyewe wakubali. Kifungu chochote cha Katiba kinacho husiana na freedom ya wananchi

hazibadilishwi na wabunge yabadilishwa na wananchi wenyewe.

The Bill of Rights, haki za kimsingi hazibadilishwi paka wananchi wenyewe.

Serikali zile tulizozifanya za mitaa, za wilaya, za majimbo hazibadiliki mpaka wananchi wenyewe kama wanataka kurudia ile unitary au kufanya nini, kura ya maoni siyo bunge.

Uraia, sheria za uraia hazibadilishwi ila ni wananchi. Haya mambo mengine yote wabunge wanaweza wakajadiliana na wakarekebisha.

Sasa kuna mambo fulani ambayo sisi tumeyafanya kama binadamu lakini kuna mengine ambao hatukuyaweka sahihi, kwa mfano haki za wafanya kazi hatukuzitia mkazo sana hapo. Hiyo ni sehemu ambayo bado tunairekebisha, haki za wafanya kazi.

Halafu kuna ukulima ukiangalia hapo Katiba imekwepa kabisa mambo ya wakulima na wakulima ndio wako na sehemu kubwa katika hili taifa. Hiyo ni sehemu ambayo bado tunafanyie kazi maana yake wananchi wamelalamika kuhusu corruption katika bei za bidhaa, Sugari, maziwa, etc. Kuna vitu ambavyo vinakuzwa hapa Kenya lakini zinakuwa imported halafu vinaharibu bei zetu hayo ni maswala ya Agriculture na umuhimu wa wakulima hatukuyaweka.

Nafikiri nitakomea hapo nafasi ni yenu nyinyi wenyewe ili mweze kutueleza mukituambia kama yale mliotaka tumeandika vivilivo museme. Au tumeyakosea mseme. Halafu msimame hapo mtuambia Katiba hii tutairekebisha vipi ile tukimaliza iwe ni Katiba ambayo kila mtu ameridhika nayo. Haya asanteen sana. (clapping)

**Steward Menja :** Jina langu naitwa Steward Menja. Natoka Kambe Location. Nataka unielezee kwa ufupi ile vitu hatujaelewa Chapter 19. Interpretation, nitaelewaje hii. Nataka unieleze kwa kifupi.

**Com. Swazuri :** Yale maneno ambayo yametumika katika Katiba, maana yake ni nini? Kwa mfano civil society, kila mtu ana maelezo yake lakini hapa tunaeza ukiona neno civil society hapa maana yake ni kikundi ambacho kimeorodheshwa. Kimeeleza Financial Year mwaka wa Serickali ukisikia kuna mwaka wa Financial Year mwaka wa Serikali ujue unaanza tarehe 30 June mpaka mwaka mwagine tarehe 30 June. Hiyo ndio maana ya interpretation. Ni kama ile dignation of tongues, sawa.

Haya mwagine. Jina lako?

**Nicholas Safari :** Mimi jina langu naitwa Nicholas Safari. Kutoka Kambe Ribe Location. Swalii ni kwamba mmesema ya kwamba wabunge hawatachaguliwa kama Mawaziri hawa mawaziri watachaguliwa kivipi?

Tena nikiendelea kuuliza swali lingine. Ni kwamba pengine mimi nimesoma sana na pengine nina degree ama pengine najua mambo ya upasuwaji katika Kenya nzima mimi ni mtu wa kwanza. Kama pengine naitwa Dr. Chibule Wa Tsuma na nimepigania ubunge nimepata mimi ule ubunge. Je kunawezekana mimi pia kuchaguliwa kam waziri au la.

Swali la tatu linasema ya kwamba hawa watumishi wa Serikali watachaguliwa kivipi? Kwa sababu mara ingine unaona watu wameingia ofisini umfundishe kazi lakini hatuwezi kuelewa ikiwa kipengeli hiki kilirekebishwa jinsi ya kuchaguwa hawa watumishi wa Serikali au bado hajarekebishwa. Ni hayo to.

**Com. Swazuri :** Tulisema kwamba kuna waziri wabunge, kwanza wabunge hawatakuwa mawaziri. Kwa hivyo hata kama wewe unajua upasuaji lakini ukienda mbunge ujue wewe kazi yako ni ubunge tu. Ile kazi ya uwaziri wa afya hutaipata. Unaewela hapo. Sasa basi uamue uwe mbunge au uamue uteuliwe kuwa waziri. Sasa hawa mawaziri watateuliwa na waziri mkuu. Waziri Mkuu ndio ataangalia nataka waziri wa Afya. Atatafuta mtu ambaye Kenya nzima afikiria anaweza kuwa Waziri wa Afya. Jina alipeleke Bunge. Umeelewa? Sasa wake huwezi kuchaguliwa kama si mtu ambaye wajulikana na kazi zako umefanya vipi. Sasa wale wabunge watajadiliana Bunge la chini ipelekwe Bunge la juu wajadiliane huyu mtu hafai au wafaa kuwa waziri wa afya. Hivyo ndivyo ndio tutafanya kwa mawaziri.

Halafu wafanya kazi wa Serikali umesema kwamba serikali za mitaa hizi ndogo hizi hapo serikali ambayo itakuwa na jukumu la kuandika wafanyi kazi wake ni Serikali ya Wilaya. Hiyo itaandika wafanyi kazi wake. Ina ruhusa ya kusema hawa wote walioko nendeni zenu, twaanza afresh. Tume wapa nguvu hizo. Wale wataandika watu wao. Serikali ya mkoa pia ina ruhusa ya kuandikwa wafanyi kasi wake laking wale wafanyi kazi wa Serikali kuu maana yake ina sehemu yake yakufanya. Ile ina uwezo wa kusema okay huyu twampeleka mahali fulani akafanye kazi fulani. Lakini uwezo mkubwa sasa hauko kule juu. Huko Serikali ya Wilaya au Serikali ya Mkoa.

Haya mwingine? (**end side B tape 1**)

**Kalume Tunje :** Jina langu ni Kalume Tunje, mimi natoka Kambe Ribe. Nilikuwa na maswali mawili ambayo nilikuwa nataka tufafanuliwe. Kwanza ni kuhusu hizi sehemu zinaitwa DIDs District Information and Documentation Centres. Kwa hivi sasa katika Draft yenu nimeona kuwa mmezitaja katika District level. Kuwa kutakuwa na hizi hivi vituo ambapo mtu akitaka information yeyote anakwanda kule kuipata. Mimi ningependelea kama hivi vituo vingekuwa mashinani. At the grassroots level, at location level pia at the Divisional level kwa sababu mimi nina hakika mambo mengi yanaharibika kwa vile watu hawana information. Mtakuja shutukia kuna senti semekuja za msaada mnakuja kushutukia kuna ng'ombe zimekuja za msaada, na hali hiyo ni plan ilikuwa hapo for almost 6 or pengine mwaka mzima. Lakini kwa vile kile kituo kiko mbali hakuna kituo karibu ile information hamuipati na pia hamtafaidi.

Swali langu la pili, ama comment ni kuhusu ardhi ambayo haitumiki vizuri, ninaona kuwa mnasema ardhi ambayo haitumiki vizuri

itakatishwa kodi, itakuwa taxed. Mimi ningependa kuuliza hii tax mutaiangalia kiwango chake kulingana na ule umuhimu wa ile ardhi ama just the acreage, na ikiwa mta-tax mtawapa muda fulani wale wenye ile ardhi ili waweze ku-raise ile tax ama mtasema ukiwa defaulter wa tax fulani basi ile ardhi itachukuliwa? Kwa sababu mimin ninaunga mkono kwa vile kuna tracks of land which are idle lakini katika hii tax ningependlea sana tuwe na mwongozo ile mtu ajue mimi niki-default nitapewa muda fulani na ardhi yangu ina value fulani kwa hivyo tax yake itakuwa kiwango fulani. Asante

**Reuben Tsumah :** A point of information. Ni hivi ndugu zanguni. Kina mama kina baba, na Tume ambayo imetoka Nairobi kuja kuwa nazi hivi leo siku nzimba nafikiria, tafadhalini nimesikia watu watatu hapa wakisimama wanatoka Kambe Ribe. Haya ni makosa, hakuna Kambe Ribe kuna Ribe na kuna Kambe, maana yake Ribe ina diwani wake na Kambe ina diwani wake na hizo ni location mbili tofauti na machief pia wako tofauti kwa hivyo tafadhalini kutoka leo, nyinyi mnaotoka Kambe, nyinyi mnao toka Ribe mafanue kwamba ukiwa unatoka Kambe unatoka Kambe na ukiwa unatoka Ribe unatoka Ribe usije ukaguzia hiyo nyingine. Asanteni. Inasemekana ni taje jina langu. Mimi naitwa Reuben Tsumah. Asanteni.

**Anderson Nyachi :** Mimi ni mzee wa kazi naitwa Anderson Nyachi kutoka Ribe Location. Maswali yangu ni matatu kwa manne lakini kama inaendelea naweza kuwajishwa. Mimi tumefanya ndugu zangu kwanza nataka kutoa sifa kwa hii Katiba mpya. Mimi nashukuru sikutazamia vile jinzi ambavyo tulifanya hapa lakini labda kwa huu uzee sikusikia vizuri, pale mahali pangu sikuguziwa. Labda hii mmeandika Kingereza mkileta Kiswahili ndio nitaelewa. Mbona hamkunitajia mimi vitu vinaitwa Federal Government? Yaani Majimbo. Regional Assembly sikusisikia, nitangoja hiyo ya Kiswahili, number one.

Number two, ni Katiba hii mpya sisi tulikuwa tumezungumza hapa sikuelewaka lakini nataka mnielewe. Karne hii ya leo wasichana wa Pwani ama Kenya nzima watiwa mimba tu na hakuna hatua ye yeyote ukienda kortini wapi, watoto wale naletewa mimi, na mimi nina wasichana tisa kila mtoto wacha na watoto watano kule kwangu nyumbani na mimi sina kazi. Ile namna ya kutoa mimba mtoto wako ama wangu na serikali isichukuwe chochote, watoto wa leo wasichana hawaolewi. Kwa nini hakuna protection, ningefanya kama kuomba.

Number three, nafikiri up country huwa ni afadhali lakini hapa Pwani wamama hawarithi mali ya wazee wao. Na mimi niko karibu kuwaridhisha watoto wa kiume na wakike. Katiba mpya yaweza kutia clause kwamba wamama waridhi baba zao. Nafikiri hapo leo maswali mazuri. Sio kama vile nilikuwa na moto zamani lakini sasa umepoa.

Jambo jingine ni lile la wageni hawataruhuziwa either kurithi ardhi, lakini ukiangalia nyuma tayari ufikirie zile ardhi tayari zilizochukuliwa ama kununuliwa na Waarabu, wale Mazurui, Mwambao wa Pwani na Missionaries wamekapa ile Kisauni, Mazeras, Shichombu, Ribe, Mapa ya Nyundo, kwa miaka na miaka yaani in the past tumezungumza in the future, siku sijazo, je wale miaka mia mbili mia tata za Waarabu wameketi na sasa hatuna ardhi, na Missionaries wako pale, pale Ribe na fungo wapi ile miaka mia tatu ni ya nini mtawafanyaje wale wa zamani? Are you going to revoke? Mtafutilia mbali yale maneno ya wao sasa hakuna land. Nafikiri kuna mengine lakini nitanyosha mkono baadaye kuwapisha hawa. (clapping)

**John Kasuku Mwamsonga :** Asante sana, mimi pia jina langu ni John Kasuku Mwamsonga ni Councillor Jipana ward. Nilikuwa na mawili moja kidogo limeguziwa, na nikuhusu hii Serikali ya Majimbo. Tulikuja hapa tukatoa proposals zetu, kwamba Serikali ijayo iwe ya majimbo lakini hatukusikia hiyo, labda pengine kutakuwa na marekebisho zaidi wakati mkiendelea. Hili ningependa tena kushukuru ile Tume ya Katiba kwa kazi yao nzuri amba o wamefanya, hata ingawaje upande mwingine wanapigwa vita lakini sisi wananchi huku wa chini kabisa tunaipongeza ile Tume ya Katiba.

Inginge ilikuwa ni kuhusu hii Village Councils, na tungependa tufafanuliwe zaidi itafanya kazi vipi? Asante sana.

**Com. Swazuri:** Kwanza tutaanza ba yule mtu wa Kalume, District Information Centres amependekeza kwamba ziwe kwenye Division na Location. Hiyo Tunakubali tutakwenda turekebishe hiyo.

Halafu idle land, ile ardhi ambayo haitumiki vizuri tumesema kwamba Serikali Bunge lipitishe sheria ambayo itawezesha ardhi ambayo haitumiki itozwe kodi na mathumuni yake ni mara mbili. Kwanza tunataka maendeleo kwa hivyo ardhi ni lazima iwe inatimiza ile kuendeleza sehemu ile. Pili tunataka ardhi iwe ina mwenyewe ambayo anaitumikia kuondoa ile shida ya absentee landlords, wale waarabu ulikuwa unasema. Kwa hivyo hatujajua ule undani haswa ile ardhi itatolewa ache, itatozwa kodi either kwa wingi wake au kwa uwezo waka wa rutuba yake. Hiyo tumesema tutawacha kwa wale watu amba o watafanya details ule undani zaidi wataangalia lakini haswa ardhi itatozwa kodi ikiwa ni kubwa kupita kiwango fulani. Na hatujakubaliana kile kiwango ni kiwango gani. Lakini kiwango cha ardhi eneo lililo nalo lazima kuwe kuna kiwango fulani ambacho ukizidisha hapo na haujakitumia, hapo tutatoza kodi na tutatoa muda, tutafanya valuation halafu tutatoa muda wa kodi hiyo.

Halafu, Anderson, mzee wangu pale na Councillor hapa amesema kuhusu Federal Government. Tuseme hili jina majimbo haliko hapa, hili jina ambalo mwalitafuta majimbo matalitafuta sana hapa maana yake halimo. Kwa sababu kwa vile ambavyo neno majimbo limeeleweka kimakosa kwa watu wengine wa Kenya. Hao wamefanya ieleteke kwamba ukisema Majimbo ni kwamba wataka kufukuza watu wa sehemu fulani kutoka sehemu fulani. Sasa kwa sababu ya kwamba limejaa na sumba ile, wale wanao sema vile ni wengi, sasa watu wote wasema tukitaja majimbo yajulikana wataka kufukuza watu fulani. Sasa ndio neno lile kwa sababu tunasikiliza wananchi wote tulijua tukilitia pale wale watasema hee, hee wale wamerudisha yale mambo yao. Kwa hivyo hata ukilitafuta wapi hulipati, maana yake twataka kuondoa kule kutoelewa kwa watu kwamba majimbo siyo vita.

Na tulieleza kwamba katika mijadala yetu tukaangalia kwamba tumeona Serikali nchi nyingi ambazo zilikuwa unitary zimeenda kwa Serikali za chini zaidi. Hii nchi mifano yake haina ifadhi. Lakini hatukuona Serikali ambayo zamani ilikuwa ni majimbo yakaja yakawa moja. Hivi sasa wananchi wengi wanataka self determination, dunia nzima si hapa Kenya peke yake watu wanataka services karibu. Sasa tukaona badala ya kutumia neno lile majimbo tutaweka zile viwango zike sehemu ambazo Serikali wananchi watakuwa wanapata huduma zao. Na hakuna jimbo kubwa kuliko jimbo ambalo ni la village. Kile kijiji

chenu, si Mwamba ya Nyundo kile, nyinyi pale pale mna assembly yenu. Wajumbe wakusanya pale mwaamua mambo ya Mwamba ya Nyundo. Haya haitoshi kuna location za Fafani, pia nayo wabunge watatoka pale katika Mwamba ya Nyundo watatoka wapi, vijiji kumi wataunda Serikali yao. Hilo ni jimbo lao pia, haitoshi wale wale watachaguliwa pale watachaguliwa kwa district nzima, Kilifi District wana Assemby yao. Hizo details sikusema lakini kuna Assemblies pia watakutana wale, District wana Assembly yao, Bunge lao. Halafu hiyo yaitoshi bado kuna Bunge la Jimbo, province, mkoa, kulingana na ile kuwa minane ya sasa hivyo. Kwa hivyo ndipo lile jina lakini kwa sababu limeeleweka vibaya halikuwekwa pale. Maana yake tukilitaja hapo litaleta vita lakini wote wanakubali kwamba Serikali ya unitary ya kwamba iwe Nairobi pekee yake, haifai.

Watu wote wamekubaliana sasa badala ya kwamba tuseme tuipeleke kiwango fulani pekee yake wengine wakasema pia hiyo haitoshi waweza ukaweka jimbo tukawa na dictatorship pale pale kwenye jimbo hapo hapo kwenye jimbo kama kuna viongozi, kuna kabilia fulani ndio wenyewe, yawezekana hiyo, hata hapa Pete yawezekana hapo. Tukasema kwamba ni Jimbo la Pwani halafu tukaingia wenyewe wa Pwani sasa, wakawa wako pale ndani. Mkambe akisema hasikiliza, Mdigo akisema hahangaliwi, mtaita akisema haangaliwi, itakuwa pia ni hiyo sasa sisi tunasema, tunaenda chini zaidi ya hapo. Kwa hivyo hilo neno kama mwatafuta majimbo, mmekuja kusikia kama kuna Serikali ya Majimbo, yipo lakini jina zilo.

Halafu kuna swala la msichana, wasichana wanadungwa mimba, mimba ovyo ovyo, mimi nilikuwa naona utanilifikisha kwa upande wa urithi. Lakini umesema tu tabia ile. Tabia ile sasa tumeangalia kwa upande wa Bill of Rights. Ukiangalia sana hapo kuna vikwazo tumeweka pale, kwenye Bill of Rights, iko hapo. Lakini ukileta upande wa urithi wasichana tunesema wana haki yao ya kumilki mali za wazazi wao, wataenda wapi? Tusijidanganye wakati ya kwamba msichana lazima aolewe. Sasa siku hizi hakuna. Wenyewe wanaamua tu wapate watoto na wasiolewe. Kwa sababu waume wakuona wanawake siku hizi ni kidogo, sasa atakuwa amesoma amepata kazi yake, amepata mimba, amepata mtoto lakini ataenda wapi, kwa baba yake, tuko nayo pale pale. Sasa utamunyima huyo atakwenda wapi. Yule bwana aliye huyo mtoto hana habari kabisa wala hataki maneno ya yule msichana tena. Anatafuta mwingine, sasa hawa ni wengi, hatuwezi kutu-blind ukasema ni uwongo hakuna, ah, ah, ni wengi, kila nyumba yuko hapa hata hapa kila nyumba utakuta mtaa fulani wasichana kumi wana watoto wao na wako pale pale nyumbani. Sasa hatuwezi kujificha tukasema ah, ah, it is not a problem hiyo. Wala si wakati wa kusema ni aibu. Umepita wakati huo sasa. Maana yake wafulana ni sisi wafulana wakuoa na kuwa ku-divorce kama mzee wangu alivyokuwa kama wewe, siku hizi ni kidogo. Na hawa wasichana wa kuolewa wakaishi nyumbani miaka 40 pia nao ni kidogo. Sasa itabidi wazazi wakae na watoto wao na watoto wa watoto wao, wajukuu wao. Ukitaka usitake, ni hivyo sasa, sasa kwa sababu hiyo tumewapatia ruhusa kulingana na mila zao, kama yule msichanga atakaa pale na ni mtoto wako atarithi kwa nani kama si kwako? Kama mila yako yaruhusu apewa, haya huyu mpaticie maana yake hana pahali pa kwenda yule. Kuna mila zingine zinasema atapewa ruhusa ya kujenga nyumba tu. Lakini kama atakaa kuuza ile sehemu ya shamba hana ruhusa. Hiyo pia ruhusa ya kujenga nyumba na ajenge maana yake atakwenda mahali. Kwa hivyo hiyo tumerekebisha hapo.

Foreigners, hawa wageni tunesema kuna wale wa miaka elfu moja na, wageni ambao walipata ardhi. Walichukuwa ardhi miaka elfu moja na mia tatu yaliyopita. Sasa tunesema, ukiangalia kifungo kile kimesema kwamba, ni kifungo number kumi na

moja, imesema kwamba katika miaka miwili hii baada ya Katiba hii kufikishwa, Bunge litapitisha sheria ni lazima Bunge lipitishe sheria katika hiyo miaka miwili kwamba to review and assess all claims, ichunguze na iangalie na ikiwezekana ifutilie mbali au irudishwe kwa wenyewe mikataba ya ardhi iliopita yote, yiko hapa sehemu, section 4 chapter 11. Tenue of land, ni kifungo number 235 Sehemu ya 4 (b)(i). Tumeeleza hapo kwa hivyo hata tumeleza Bunge litaamua waende nyuma miaka mingapi? Kama ni miaka elfu moja, kama ni miaka mia tano kama ni miaka mia tatu waende nyuma mpaka wahakikishe kwamba tunaweza kuuliza uliza mpaka tukajua ile ardhi yetu ile ilichukuliwa na yule Mujerumani wenyewe miaka mia tatu iliopita walikuwa ni kina nani. Hiyo tumewapatia katika miaka miwili maana yake tukizidisha hapa tukiwapa time itapelekwa hivi na hivi maana yake watu wengi wako involved. Itakuwa hivi na hivi miaka kumi uisha na nayo kuenda hivi ni mwisho ah. Lakini tumeeleza pale very very clearly. Kwa hivyo mambo haya yatatatuliwa bwana.

Councillor ulikuwa umeuliza habari ya village council. Tumesema kwamba Village Councils tunataka, tumeleza ni wananchi wataamua hao wenyewe kwanza kama watataka kuwachagua wale au kuwateuwa village government. Na itakuwa na wanachama wasiopungua sita na wasiozidi kumi, kila kijiji cha Kenya. Kitakuwa na Bunge lake. Lakini wabunge waka hawatazidi kumi. Kati ya sita na kumi lakini kama tumeleza pale mwanzo kama mtawachagula sawa, kama mtawateua mwakubaliana wenyewe sawa. Halafu wale wenyewe tumeleza hapa wataamua wataendesha vipi mambo yao ile Serikali yao. Bora wasigeuke sheria za Katiba. Power isiwe kwa mtu moja wale wata-serve maximum miaka kumi na kadhalika. Hiyo ndio itachaguliwa bwana. Ukitoka pale katika wale wawili wawili pale wataenda kwa bunge la wilaya. Ha hapo wengine wataenda kwa bunge la Mkoa namna hiyo tukichaguana namna hiyo. Nafikiri ilikuwa maswali ni yaho Mwingine.

**Matthew Mwakamole :** Mimi naitwa matthew Mwakamole natoka area ya Kariang'ombe kule Rabai. Nimefurahi sana kusikia hii Katiba vile mliisoma lakini nilikuwa pia ni kupendekeza tu. Langu la kwanza ni kupendekeza kwamba Katiba hii mimi binafsi imenifurahisha na kwamba ingekuwa uzuri Katiba kama hizi au mambo kama haya yawe yanaweza kufundishwa mashulenii ili kwamba mtoto akikuwa awe anajua haki yake. Hiyo kwanza.

Pili, jambo lingine ni kwamba nimesikia kuhusu Kamati zile ambazo zitapunguza mishahara ya Wabunge, lakini sikusikia ya kwamba kuna kupunguza mishahara kwa sababu ile mishahara ambayo inapatika hivi sasa hata ni kufuru. Ile mishahara ni ya kufuru maana yake wanapata mishahara yakufuru mwingine hana hata shilingi ishirini yakutoa harambee na mwingine ana million tatu. Kwa hivyo hapo mimi nilikuwa nataka kuchangia kuhusu jambo hilo.

Jambo lingine ni kuhusu haki za watoto. Hatukusikia ikitiliwa mkazo kwa sababu mtoto anatakikana asome kuanzia hata kuanzia nursery, primary mpaka university bila matatizo yeoyote. Lakini unakutu matatizo kama mtotoa anapita mtihani ama amepita mitihani yake lakini hizo nafasi pengine hata hatazipata. Pengine wazazi wake ni masikini. Mimi mwenyewe ninayesema nilipata shida hiyo ambapo mtoto alipita kwenda Alliance ilibidi nifanye harambee, na nilipofanya harambee ile pesa ikawa haikutosha, ikawa shida sana kusomesha. Kwa hivyo mtoto alimaliza kule lakini halafu baadaye ikakuwa kwamba kwa sababu uwezo ulikuwa ni kidogo nikakuta kwamba mtoto amemaliza lakini bado nadaiwa lile deni nililipe. Kwa hivyo naona

kwa Katiba inatakikana mtoto alindwe katika hali ya kielimu.

Jambo lingine ni kuhusu haki za wazee. Wazee sikuona kama haki zao zinatoka vizuri pale. Utakuta mimi nime-retire katika kazi za Serikali lakini utakuta ya kwamba baada ya ku-retire utakaa miaka miwili, mitatu au sita ndio upate maruburubu yako. Ile pension kuipata haina cha kuongezeka ni pale pale ulipoipata kama ilikuwa ni shilingi elfu moja na mia tano ni hivyo hivyo. Kwa hivyo mimi naona kwamba pia haki za wazee zifikiwi. Mimi siongezi mengi.

**Ngala Kibanzu :** Mimi kwa jina ni Ngala Kibanzu kutoka Kayafungo. Kwanza nataka kutoa shukurani zangu na mapendekezo ambayo imesemwa hapa kuhusu marekebisho ya Katiba. Nilikuwa nikuulize lakini umejibu mwenzangu mwingine. Langu tu ni swali kwamba pendekezo hilo lenu ni nzuri na uchaguzi ni mwaka huu. Pendekezo hili litaingia katika uchaguzi ya mwaka huu ijayo au namna gani? Kwa sababu, kuna msema ya uchaguzi utakuwa mwaka huu na Katiba ya zamani.

Sasa ikiwa ni Katiba ya zamani karibu mambo yote uleyzungumza hapa yale mazuri mazuri hayako. Na wale wakubwa wetu huko wanapendekeza kwamba uchaguzi ufanywe kwa sheria ya zamani, hilo ni swali nauliza nijibiwe itakuwa vipi maana yake ikiwa itafanywa na Katiba ya zamani karibu mambo yote uliyosema hapo haitafanyika. Mimi kama nilivyopendezwa, ombi langu linataka uchaguzi ujao ufanywe kwa sheria ya Katiba hii mpya.

Pili, kuna Serikali za vijiji, hiyo imenipendeza sana, kutoka location imenipendeza na za Wilaya. Sasa hii ya wilaya umetuguzia mahali pa wabunge hata ukasema kiwango chao ni afanye mtu wa Form Four ambaye pia ali-pass vizuri, lakini hukuguzia mimi ni Councillor bwana. Na sisi ndio wazee. Nimefanya hiyo kazi ya U-Councillor ikiwa watu wa Kayafungo watanipenda. Maana nyinyi mlikuwa hapa sisi tukapendekeza, na nimeona mazungumzo yako unatujuibu yale tulio pendekeza na kufafanulia ile tunasema na nyinyi sheria mkasema badala ya hivi ni hiki. Sasa hapo nataka pia utuambie, mimi nina umri umepita hilo ulilosema kwamba mtu atakeyepigania ubunge, iwe mwisho ni miaka 70 na wengine huyu unamuia mkongwe hapa amepita miaka hiyo, nataka ufanue hizi Serikali za wilaya. Kama ulivyo andika hapa vinaanza vijiji location na wilaya hii ni Serikali ya kivipi hawa madiwani wako upande kani kati ya Serikali hii. Asante.

**James Indimuli :** Asante, mimi naitwa James indimuli na ninatoka hapa Kaloleni. Maswali yangu mawili ya kwanza Umetaja bunge inaitwa National Council ile ya watu mia moja. Ningependa utufafanlie nani attachagua sababu moja katika every district nani attachakua hawa wagunge wa National Council.

Ya pili, is just a comment. Nilishutuliwa kusikia ya kwamba mambo ya kilimo na mambo ya wafanyi kazi ilikuwa haikusemwa katika Katiba hii. Hiyo ni oversight, au hamkuwa na wakati wakutosha kwa sababu uchumi wote unategemea Kilimo ikiwa hii inaweza saulika sijui ni kwa nini inaweza kuwa imesaulika. Asanteni.

**Tembo Kakunde :** Kwa majina naitwa Tembo Kakunde kutoka Kaloleni. Ningetaka kuuliza kuhusiana na mashamba, umetusomea na nikasome pia kwa mtu hawezi akapokonywa shamba lake kwa sababu labda kuna madini fulani pale ndani.

Lakini ukifwatiliza kidogo pale chini tunaambwa kuwa Serikali inaweza ikachukuwa lile shamba ikiwa inaweza kuitumia kwa manufaa ya watu wengi, je hapa sheria itaelekea upande gani kwa Serikali au kwa wenyewe shamba.

Pia kuhuziana na mambo ya kuoana hapa mumeweka kipengele kuwa watu wanaweza kuoana kutegemea makubaliano kati yao wenyewe. Je hii, hiki kipengele hakiweki nafasi ya watu wa jensia moja labda kuoana kama ilivyo kule Marikani au Ulaya. Asanteni

**Com. Swazuri :** Let me confirm. On the family every person who is at least 18, Article 38 (3), have the right to marry, depends upon the free consent of the parties, labda waume wataoana.

**Abdalla Baya :** Asante, mimi kwa majina naitwa Abdalla Baya kutoka Mwanamwinga. Mimi ningependa kuangaza kuhusu uhuru wa kiraia. Tumeona kwamba katika sehemu hii ya uhuru wa kiraia, Umekuwa na jambo kwa kusema kweli upande wa kina dada hasa, upande wa mavasi hapa naona kama nafasi hii imekuwa na mchango mkubwa sana kusababisha mambo ambayo si ya kurithisha. Kwa sababu utakuta mara nyingi jinzi wanavyo jipamba dada zetu inakuwa ina mchango fulani kwa vituko kama unajizi kupata nafasi ya kupenyeza pale ndani yake. Na hili ni jambo ambalo liko dhairi mtu akiwa pengine amefaliana vivu mtu akiwa ana mawazo ya kufanya kitendo kama cha unajizi cha kiuhalifu namna hiyo siyo rahisi. Lakini njia wanaojiweka madada zetu inakuwa ni kama wanaji-advertise na tunaona kama kuna udhaifu kwa kila kiumbe unaona unaweza kustahamili na kuna wengine ambao hawawezi wakastahamili kwa hivyo uhuru wa kiraia tunaona kwamba upande huu umekuwa na mchango mbaya, tena mbaya zaidi. Hilo ni swali langu la kwanza ambalo ningependa Tume ijaribu kuangaza, uhuru wa kiraia.

Pili, ni kuhusu vyombo vya habari haza saidi runinga, inatubidi sasa wenyewe runinga tuwe na wakati maalum wa kuangalia na kuna wakati ambao inabidi tufunge tuachie labda rika fulani liangalie. Kwa sababu zinaleta programme zingine ambazo haziruhuzu mtoto na baba yake ama mtoto na mama yake wawe wanaweza kuona wakati za runinga kwa wakati mmoja. Hilo ni jambo ambalo pia ningeomba Tume iangaze uhuru huu wa vyomba via habari.

La tatu, ni kuhusu usani tumeona kwamba wasani wengine haza waimbaji miziki, wamekosa mwelekeo wamechukua nafasi hii kutumia usani wao kutunga maneno ambayo hata kama ume-tune muziki kwa radio, utatamani tu hiyo radio hata kama ni battery zishe maana yake inafika mahali ule ujumbe ambao huko kwa ile muziki si ujumbe wa kuridhisha, si ujumbe wa kunufaisha mtu kwa njia moja ama ingine ile. Ni ujumbe tu muusani yule amejifaidisha pengine anajua kwamba kuna kikundi ambacho hakiwekwa yale maneno ambayo si ya kisawasawa upitia watu kama hao atatengeneza soko kwa hivyo hao ningeomba Tume ijaribu kuangaza mambo kama hayo. Asanteni.

**Alfred Dunda :** Asante sana. Mimim naitwa Alfred Dunda na nataka nizungumza kidogo kuhusu mambo ya ardhi. Maana yake tukitazama sana ardhi ndio ambayo kwamba sana huleta mizozio na hapa inasemekana kwamba ardhi ni ya Wakenya

wote. Sawa ni vizuri lakini, ningeona ingekuwa vizuri kama ni Wakenya wote lakini wakanya ambao wanaishi katika sehemu ya ardhi hiyo ile tusiwe na mkonganisho kwamb hawa wanatoka kule, wote ni waKenya. Lakini sasa kama kwa mfano hapa ni Pwani. Ardhi ni ya Wakenya lakini Wakenya ambao wako hapo. Kwa hivyo mimi naona ingekuwa ni kutu bora kwangu. Asante.

**Eli Simeon Kondo:** Mimi naitwa Eli Kondo natoka location ya mariakani. Swali langu lilikuwa ni moja katika ile utekelezaji wa Village Council.. Kama sasa Chief atakuwa ameondolewa, na pengine DC na hizi village council ambazo mmesitaja zitakuwa zikifanya kazi, ikiwa pengine mmejadiliana nataka kujua, itabidi sasa kama mtu hakutosheka anaenda vile vile kwa taarafa mpaka afike kwa mkoa ama namna gani?

Na kitu cha pili ambacho nataka kuchangia ni hii habari ya elimu. Nimeona hata mimi ni mmoja wapo nilichangia kwamba hii elimu ya watoto iwe ya lazima na ya bure. Naona mmeandika ambayo na shukuru sana imekuwa, lakini ule utekelezaji hauonekani kama unawenza kufanyiwa na nani mpaka kweli watoto walazimike kwa sababu ya wale wazee ambao wana pesa nydingi lakini wame-neglect watoto wao. Hatujui watafanyiwa nini mpaka tuone kwamba kila mtoto anazaliwa Kenya anapata nafai kama wengine kwenda sikuli.

Swali langu lingine ambalo ni la tatu ni hii Katiba ambayo tumeifanyia bidii sana. Iwe katika marekebisho mazuri. Lakini sasa tunaona kwamba tumefungwa mikono kwa ule upinzani. Ikiwa sasa tutaweza kwenda kuingia kwa uchaguzi kwa Katiba pengine hii hii, na yule ambaye atashikilia atakuwa hana, ana powers zile zile ambazo hapa mmesema vizuri sana ingekuwa hana powers, akiwa na powers na aifinye mpaka miaka mitano ijayo, tutafanya nini pale. Iko powers za hii Commission kulazimika kwamba imalize kazi yake na ipitishe Bunge kabla ya uchaguzi au kutafanyika nini tuone kwamba imekamilika? Asante sana.

**Com. Swazuri:** Nitaanza upande wa mishahara, Tume ya Mishahara, siyo Tume ya kuongeza, mishahara, peke yake. Hiyo ni Tume ya kuchunguza na kuangali mishahara. Sasa kuchunguza kuna mara tatu either utaongeza, au utawacha pale pale au utapunguza sasa hiyo Tume imepewa kazi hiyo, sio kwamba saa yote iwe yaongeza. Kuna watu wengi walisema mishahara ipunguzwe Wabunge. Sasa Tume yenewe itaangalia itakaa iseme hapana hii million moja ni nydingi sasa tuwawekee laki mbili, kwa hivyo hiyo Tume si ya kuongeza pekee yake, tumesema ni Tume ya kuchunguza na kuangalia mishahara.

Haki za watoto mzee amejibu vizuri sana ukiangalia katika bill of rights tumesema mara mbili pale kwamba elimu iwe ni ya lazima na ya bure. Hiyo hatukuficha tumeeleza wazi kabisa, Serikali iwe na uweze itafute mbinu zozote lakini elimu iwe ni ya bure haswa ya msingi, ile ya primary school, Nursery mpaka primary school iwe ni bure na ni lazima. Hiyo tumeeleza kwa ile ya secondary school tumesema ipunguzwe bei the Government should make it accessible. Ipunguzwe bei iwe ni affordable siyo mzee kama watoto wako wafanyiwe harambee kwenda Alliance washindwe na kadhalika. Kwa hivyo yao mambo mawili tumeyaweka pale.

Kule kutekeleza, nani atatekeleza? Hiyo tumesema kwamba kuna sehemu nyingi sana katika hii Katiba ambazo zinaweka umuhimu kwamba Serikali ni lazima. Katika kila sehemu hapo utakuta kwamba tunaipatia Serikali, tunailazimisha Serikali lazima ifanye. Tena tumetoa muda ikiwa sheria hizo zote katika muda wa miaka fulani hazifanyika, hiyo ni ground moja ya kumtoa waziri mkuu. Ukiangalia katika powers za Prime Minister ni kuhakikisha kwamba Katiba inalindwa basic rights zinafanyika ikiwa hazifanyiki kwa muda fulani hiyo ni petition tunaweza tukatoa na waziri mkuu atatoka. Serikali zote, tuanze tena upya. Kwa hivyo utakuta kwamba kila ukisoma sehemu fulani inakukumbusha kwamba Katiba hii ni lazima ifanye mambo haya ni lazima yafanywe na mtu fulani, bila kufanya hivyo kifungu fulani kimetoa, asante sana. Kwa hivyo hakuna kukwepa tena hapa.

Halafu tumekwenda kwa haki za wafanya kazi, haki za wazee, nafikiri kama pale nimeeleza mwanzo, kuna maswala mawili ambayo bado tunayafanya kazi moja ni hili la haki za wafanya kazi wewe umesema haki za wazee ambao wame-retire. Mlisema kwamba mishahara ya wafanyi kazi wakaida ikiongezwa na maruburubu ya wale wazee nayo pia yaangaliwe. Hilo ni swala ambalo bado tunalijadili kwa sababu ya wakati hatukuweza kupata nafasi ya kulitoa. Sawa sawa na swala lile la ukulima, siyo kwamba ni oversight ni jingi sana na tulitaka tulizungumze vizuri mpaka tukasema hili tuliwache kwanza tutoe hivi, halafu tutakuja kujadili. Kwa hivyo kabla hatujafika kwenye National Conference, itakuwa ile draft bado inarekebishwa. Kuna wenzetu ambapo wako katika hayibu kuandika, kuna sehemu ambazo bado, hata hizi serikali za wilaya, bado kuna kikundi ambacho kinaendelea kuandika zaidi mpaka tujue uchaguzi utafanywa, yaani ile details kabisa. Bado kuna Task Force ambayo inaandika hivi. Kwa hivyo sio kwamba tumefanya oversight, lakini ni kwamba ni muhimu sana mpaka tulikuta tukifanya haraka haraka, tutakosa ile maana yake. Kwa hivyo wazee, mambo ya mishahara bado inaangaliwa.

Halafu kuna swala ambalo limeulizwa na msemaji wa pili mzee Ngala na wa mwisho kuhusu uchaguzi, kama Katiba hii mpya itafanya kazi kwenye uchaguzi ujao au uchaguzi utafanywa na katiba ya sasa. Kulingana na sheria ya Tume ambayo tuko nayo, tukimaliza hii kazi yetu tunafanya, kama nilivyoeleza hapa mwanzo tutaenda katika kikao cha kitaifa tukimaliza kikao cha kitaifa ndio tutaenda Bunge, lipitishe sheria hii mpya Katiba mpya halafu baada ya hapo ndio sasa uchaguzi ndio programme yetu ilivyo sisi, tunavyotaka sisi, lakini sisi na wale walioyoko sasa ni tofauti. Sisi twaendelea hivi wenyewe wasema uchaguzi utakuwako, tena hivi sasa na Katiba mpya, hatuna uwezo, nawauliza je nyinyi mna uwezo, hatuna uwezo sisi pia ni waandikwa kazi. Hatuna uwezo. Uwezo wetu ni kuandika hii Katiba, mmeona vile vituko tumefanyiwa mara twapelekwa kortini, lakini tumesema haja yetu mwisho lazima tufike mwisho tutoe report na tumetoa report lakini haya mambo mengine sasa ni ya wanasiwa. Wao wenyewe ndio wanaamua huko, sisi kazi yetu twafanya wao wanaamua, ikiwa watakubali kwamba wangoje mpaka tumalize halafu twende kwa National Conference, halafu ndio uchaguzi uwe, ni wao, lakini sisi tuendele na kazi yetu. Basi wao wakisema nyinyi fanyani mwaka ujao ndio itakuwa, kwa sababu wakivunja Bunge na kama umesoma kwenye gazeti hata Chairman wetu amesema wakivunja Bunge hivi sasa itakuwa ile National Conference haiwezekani kwa sababu wabunge wote ni delegates. Kwa hivyo itabidi tungojee mpaka wabunge haapishwe tena, sijui ni February sijui ni January halafu ndio tukutane tena nao kwenye National Conference. Baada ya National Conference wakipitisha ile sheria itakuwa sasa ni wao kuamua sasa itaanza siku hiyo hiyo au sisi ni watumwa tulitumwa tufanye kazi yetu, tumefanya na tunaendelea kufanya. Lakini aliyetuma sasa,

wale walituma ndio wana uwezo.

Councillors mko wapi katika huu mzururu wa hizi Serikali. Councillors wamemezwe katika District Council. Maana yake zile District Councils zitatengenezwa na waakilishi wa kutoka kila location. Kwa hivyo Councillors watakuwa ni wale watu wa District Council. Na kama nilivyowaambia bado tunarekebisha tunatengeneza details, kujua haswa Councillors wataingia namna gani pale. Isipokuwa katika miji, Urban areas wale wana sehemu yao ya local government, ma-Councillors wale watakuwa ni sawa sawa na wale wa District. Wajumbe wa District ni sawa sawa na ma-Councillors.

Halafu nani atawachagua wale waakilishi 70 wa National Council. Hawa watachaguliwa directly na wananchi. Yule mmoja mmoja, wale 70 wale kila mmoja Kilifi, mmoja Kwale, mmoja Tana River, mmoja Kitui. Wale watachaguliwa na wananchi. Kura zao zitafanywa kwamba Districts zinatakiana viti 70. Haya chaguweni wenyewe, madede yao watakuja hapa mchague. Sasa wao wenyewe watafanya campaign, mimi nasema nataka kuwa mbunge wa Kwale, wa National council, kwetu ni Kwale, kwa hivyo tutafikia mwininge naye atasema hivyo, tutafanya campaign kama hawa wengine lakini debe letu ni la National Council. Kwa hivyo wananchi wenyewe ndio watachakuwa.

Ardhi na Minerals madini ambayo inapatikana katika Ardhi. Ni kweli, ni kama kwamba tumempatia nguvu mwenye ardhi halafu nguvu zile zinaweza zikachukuliwa tena na Serikali. Hapa tuliweka hivyo kwa sababu kuna madini aina nyine ambayo yakipatikana pale hata wewe wenyewe kweli huwezi kukaa kwenye ardhi hii. Kuna mengine unaweza ukayapata pale ukachimba mwenyewe, ukafanya kazi zako hudhuru mtu yeyote wala location yoyote, lakini kuna mengine yakipatikana itakuwa ni Industry kubwa ile we mwenyewe pia huwezi ukakaa pale kwa hivyo pale lazima hata uaingiliana na Serikali, either kwa mkatiba au kwa nini lakini wewe upate haki yako na Serikali nayo iweze kupata haki yake. Kwa mfano tukikundua hapa hapa tukundue mafuta na yale mafuta umeyakundua kwa ardhi yako lakini mafuta huwa hayakai pahali pamoja utakuta kwamba yameenea area yote hii ni mafuta. Sasa itabidi lazima pale patakuwa na evacuation, watu watatolewa sana pale. Sasa ndio wale wenyewe ardhi pale ndio wataelewana na ile Serikali, maana yake wewe kama individual huwezi kununua (**end side A tape 2**)

Lakini kwa hivyo vitu vidogo vidogo hivyo waweza mwenyewe ukauza ni vyako.

Halafu kuna Section 38, ile ya kuoana jinsia, nafikiri watu wengi hata kama hatujatoka tulikuwa tumeshapata malalamiko hiyo tutairekebisha maana yake vile ilivyoandikwa, mathumuni yetu ni kwamba kuna wazazi amba huzui watoto wao wasiolewe, au wasioe. Hiyo ndio tulikuwa tulitewa upande huo tulipata malalamiko kwamba msichana amependa mvulana, ye ye msichani ni Mukiriam na ye ye anapenda mvulana wa Kikamba wazee wanasema hapana ----- watuletea mtu mwininge ambayo hata hatujui, msichana wa Kikuyu anapenda Mjaluo, mzazi wa Kikuyu anasema hapana bwana sitaki huyo Jaluo. Sasa tunasema kwamba tunataka wakipendana basi wa rangi gani wa kabilia gani hao waoane. Hapo ndio tulikuwa tumelekea upande huo, lakini kumbe imeelewaka kwamba mume na mume pia waweza kuoana, mkena mke pia waweza kuoana, ikiwa wafanya

sijaona mimi lakini nasikia wafanya, sasa hiyo tutairekebisha. Hapo ni vizuri mmetuambia.

Bwana Baya aeleza upande wa mavazi ya wasichana, kina mama ambayo yanaweza kuleta hatari kwa upande wao na hiyo imefwatana pia na Vipindi nya television na pia kuna muziki ambao unaeleza maneno mabaya. Tumeeleza katika kifungo fulani hapa kwamba Serikali, kwanza tulikuwa na ubishi hapa wa kuhusu sensorship, kuchunguza matangazo kuchunguza muziki, kabla hazijatolewa kwa wananchi. Sasa tukasema hatutaki tuwe extreme yaani tuwe tunakaza sana au tumelekeza sana. Kwa hivyo hapa tumesema kwanza katika principle zetu za kitaifa ni hatia kwa mtu ye yote kusema maneno haya ya matusi. Hiyo ni national principle tumetoa ni hatia kwa hivyo hata mwana muziki kama yatunga nyimbo yake sasa ajue kwamba sheria ya Katiba kama Wakenya tumekubaliana hatutaki maneno yamatusi. Kwanza hiyo.

Halafu pili kama ni TV programme, hata matangazo ya biashara pia tulibishana sana siku mzima siku moja tulipishana Leisure Lodge, kuhusu matangazao ya biashara ambayo yanaingiana na hizo TV programme, ingawaje tunataka wananchi wapate information tunataka wananchi wawe na uhuru wa kuabudu, lakini tuna limit ambazo lazima tuweke kwa hivyo tutakuwa na sensorship ya Vipindi ambavyo tunafikiria hatufai kwa wananchi. Radio na radio fulani ukisikia, kuna radio ambazo majina yake pia ukiyataja pia watu washtuka, jina tu la ile radio yenewe, taja, watu washtuka. Kwa hivyo yao ni mambo ambayo hatukuyasema wasi wasi lakini mtu kama ataangalia sheria utakuta ni sawa na itajulikana kama mtu atashtaki, maana wananchi wa kenya wana ruhusa ya kwenda kushtaki kwamba lile tangazo lile ni baya. Watashtaki walitoe hilo tangazo, sasa wakati wa ile kesi itajulikana kwamba Katiba inasema kigungu fulani. Kitu ambacho tunataka kufanya pengine ni kurekebisha iwe wazi kabissa kwamba ikiimba nyimbo mbaya maana ya mbaya ni ukiimba nyimbo ya matusi maana ya matusi nini, hatakikani. Hilo tutaliangalia.

Halafu ardhi – mzee anasema ardhi ni ya wananchi wote lakini ni ya wenyeji. Hiyo Tunakubali tunasema kwamba hawa wananchi pia wamekuwa defined ni kina nani? Tukisema kwa mfano tumesema kuna private land, public land na community land. Community ni wale wenyeji, tumetumia hili neno indigenous residents wapate. Kwa hivyo hakuna shaka pale. Tuiseme kuhusu ardhi ambayo mtu mwenyeji amausa kwa hiari yake. Ile mtu ye yeto aweza kununua usiyo ukalaumu. Lakini tunasema ile ardhi ambayo tunaita community land, haitapewa watu ambao si wenyeji wa pale, Katiba imesema hivyo.

Halafu swala la mzee wa mwisho hapa Village Council je, kuna-right ya ku-appeal upwards, kama vile ukitoka kwa sub chief, unaenda kwa chief , ukitoka kwa chief unaenda kwa DO, kutoka kwa DC unaenda kwa Province, mpaka sasa hapo hatukupaweka wazi, lazima tukubali, hiyo hayiko wazi. Tumesema tu kwamba Council zile ziko juu zinaweza kuamua mamlaka ya Councils zilizoko chini lakini hiyo hatukuiweka wazi kwa hivyo itabidi tuiangalie vilivyo. Nafikiri ni hayo.

Haya wengine? Tuko hapa mpaka mseme yote. Tutaanza na wanachama wa CCC halafu Chairman halafu yule bwana, yule na mzee – mzee kwa vile umeshasema utawajia wale ambao bado halafu wewe utapata suruwa baadaye.

**Priscilla Charo :** Kwa majina mimi ni Bi Priscilla Charo Councillor wa Kaloleni Ward. Mimi tu nikuuliza Commissioner ya kwamba maoni yetu mmechukuwa na Draft, mmeileta tunashukuru sana. Heko kwa kazi yenu. Lakini tunaomba mtupe wakati tuweze kuyakariri maneno haya ili mrudi tena tuje tuwaambie sahihi mambo ambayo pia tumeyaona katika hii draft yenu. Thank you.

**Cllr Japheth Baya :** I am Councillor Japheth Baya Village County Council. Nilikuwa nataka tu nirudie maneno ambayo alikuwa amesema Councillor Ngala Kibanzu, lakini katika kujibu pingine alikuwa ameongea kuhusu madiwani, elimu ya wa bunge imekuwa set, lakini madiwani alikuwa ametaja hukufafanua. Na pia pamoja na umri wa madiwani. Halafu tunasema kwamba ikiwa tutakwenda kwa uchaguzi na Katiba ya sasa, baadaye Katiba ikikamilika hivi sasa ipelekwe Bungeni baada ya ku---bungeni na ku-pass-ishwa ndivyo itaanza kufanya kazi kutoka lini tena? Kutakuwa na uchaguzi tena afresh kwa Katiba mpya, ama itakuwa ni mpaka baada ya miaka mitano kipindi hiki cha Bunge hili kimalizike ndivyo ianze kufanya kazi. Kwa ufupi nilikuwa na hayo. Asante.

**John Kalama :** Asante, kwa jina naitwa Kalama A. John. Mimi ni mwalimu hapa ni mwandishi wa Constitutional Committee. Langu la kwanza ni ombi hasa kuhusu education curriculum ya nchi hii. Hapa tunazungumzia usawa, hata katika right tunaona. Lakini tukiangalia curriculum ya education ya nchi hii haina usawa. Ndipo utakuta ya kwamba baadhi ya wazazi sisi tuliyoko hapa na wengi zaidi katika nchi nzima watoto wao wiki hii tumeshika ya tatu wako nyumbani, na kuna bahali ya wazazi ambao wana uwezo watoto wao wako shule kwa sababu curriculum ziko aina aina, kuna zile zina-favour kina Dr. Swazuri na zile ambazo zinakalia kina Kalama. Kwa mfano kuna bahali ya mashule katika nchi hii ambayo yanafwata curriculum ya kutoka nje.

Ndipo utakuta ya kwamba shule hizo haziguzwi na wale ambao wako mamlaka wakati huu. Wengi watoto wao wanasoma katika shule hizo. Tunapendekeza hivi ikiwa inawezekana. Nyinyi wenzetu ambao mna udhehefu wa sheria, huu usawa uonekane katika elimu. Isiwe hawa wanaweza kukaa nyumbani mpaka wale wangwana watakapo kaa waamue vlivyo sawa ndipo warudi madarazani.

Pili, ikiwa ni usawa uonekane basi Serikali inapata mamlaki, ionekane ya kwamba inawajibika, si Serikali ambao itakuwa leo ina fwatana inakaa unazungumza nayo mnapatana halafu kesho asubuhi anageuka anasema hapana hatukusema hivyo, sasa kule kuhajibika kwa uongozi pale tunautilia mashaka.

Haya mengine yaweza kuwa kama point of observation kutokana na wengine walivyosema. Katika death sentence. Tumesema ya kwamba leo tumependekeza kusiwe na sheria ya kumhukumu mtu kuuwawa, okay, lakini ikiwa mtu yule ameua anajulikania ya kwamba yeche ana vitendo vya kuuua kuna jamaa waitwa Mungiki wanaweza kuchukua barabara hii na wakasema ni yetu. Pengine tungepata mwangaza hapo. Maana yake yule anayeua si dhani ana haki ya kuishi kwasababu tunataka kubadilisha Katiba tu.

Pia katika uchaguzi umetuambia ya kwamba Tume haina mamlaka. Mamlaka yana wananchi. Sisi hapa tukisema ya kwamba

tumesema tunakuambia wewe ama tunayaambia Tume wananchi wa Kaloleni Constituency wanasema, wanataka uchaguzi ujao ufanyiwe kwa Katiba mpya, hata kama mtu hatajukuwa hatua kusikia nako hasikii? Siatasikia? Maoni ya sisi wengi yakiwa na ya fwatishwe tunataka uchaguzi ujao ufanyiwe katika Katiba mpya.(clapping)

**Com. Swazuri :** Wajua shida ya hapo ni kwamba watu wanataka uchaguzi mwaka huu, tena wanataka uchaguzi na Katiba mpya, ampapo kidogo hapo, vitu hivyo vitaingiana lakini kwa kulazimika sana, sasa kama wengi wetu wanasema wanakubali hata kama ni mwezi mmoja saidi lakini (inaudible) (laughing)

Sikia hili swala sitalijibu kwa sababu limikatalika pale. Kwanza kulikuwa na ubishi wa kwamba uchaguzi ufanyike mwaka huu hatutaki Moi aongezewe hata siku moja, hamkusikia hivyo? Hata siku moja, Tume iliposema sasa inataka muda iongezwe ile uchaguzi ufanyike baadaye, watu wakasema, no, hata siku moja asipewe. Ikifika tarehe 29, aende zake kwa njia zote, jamani Katiba itakuwa bado, ah, ah, sisi haki yetu iwe asiweko. Sasa Katiba itakuwa tayari baada ya National Conference lakini bado kuna vitu kama haya mnauliza hapa tayari.

Kuna mambo ambayo lazima tuyatengeneze kwa sababu kwa mfano tunaondoa Provincial Administration huwezi kuwaacha wananchi bila ya mtu wa kuwaangalia pale kwenye village. Ni lazima, tunaweka 90 days kwamba, juu hizi structures zifanye kazi 90 days. Mtoto amekufa, mtoto amezaliwa birth certificate hatujui itatoka kwa nani? Mtu amekufa death certificate tutapewa na nani? Kijana ameshikwa amepelikwa jela itakuwaje. Vitu vile haviwezi kukaa bila Serikali sasa tunataka muda tuvitengeneza, tuna hizi Commissions lazima Tusiweke tayari, vile vyote vitataka muda kama amesema Councillor hapa lazima kwanza tuwaeleze wananchi kwanza haswa Katiba mpya inasema nini. Ili wakiondoka hapa wakiona askari pale wanajua wameona mtumishi wao. Maana yake saa hizi ukiona askari wewe kidogo tayari unajua kuna problem hapa. Patakuwa na shida hapa sasa watafute the next nearest step. Paka tuwfundishe wananchi paka wajue ukimwona yule unaweza kumtuma, nenda ukafanyie hivi na akaenda.

Watu wamesema wanataka uchaguzi mpya na Katiba mpya sasa hivi na wajua hapo kwa mkweli usimama na kwa muongo pia usimama, hiyo maneno mawili lazima tuangalieni hapo. Ikiwa tunataka Katiba mpya mkubali kwamba uchaguzi tutachelewesha hata kama ni kwa mwezi moja angalau tuweke structures ziwe sawa. Lakini mkisema kwamba 29<sup>th</sup> December Katiba mpya 29<sup>th</sup> December uchaguzi, kidogo naona hapa, haiwezekani. Lakini mkisema lazima atutawale hata kwa siku moja alioyopo na lazima, twawapatie hivi hivi lakini iko na vitu ambavyo havitakuwa sawa sana, sasa uamuzi ni wenu lakini kuwapelekea habari kwamba wananchi wanataka uchaguzi na Katiba mpya habari hizo tutazipeleka sana. Haya endelea na swali lako la mwisho.

**John Kalama :** Sasa katika ule muda wa kupongeza, nathani ninyi watu wa Tume mngetupa mwongozo, mwezi moja unawatosha ama mwezi miwili? Ama minne? Ili tuweze kusema ya kwamba, haya kakuna neno sisi tuko tayari, tuko tayari hata muda kama ni kuongezwa.

La mwisho pengine lingekuwa nataka kuliuliza kama sijui chochote. Umetangulia kusema wa kwamba hakutakuwa na Wabunge ambao watakuwa mawaziri. Pengine kama layman niulize, mawaziri hawa watatoka wapi? Na ikiwa hawatakoka katika wale wabunge hamuoni ya kwamba hatukakuwa nafasi pesa kuingia mikononi ili mtu apate kuchaguliwa kuwa waziri, maana wale wana uwezeo ujasiri wao ni uwezo wa kifedha watasema, tumepata nafasi. Lakini wale ambao wana uwezo wa kiakili na ujasiri wa kimaarifa hawana fedha watufungiwa mlango. Je hapo napo mmeplaangalia vizuri. Asante.

**Lucas Mwagangi Munga :** Mimi ni Lucas Mwagandi Munga, kutoka Chibana Location. Swali langu ninauliza upande wa sheria hawa wafungwa ama hawa suspects, kwamba hawa wataptiwa accommodation mzuri, mavazi mazuri, chakula kizuri, Je hawa nao ambao wameshapatikana na hatia hata wamefungwa sheria itakuwa ni hiyo hiyo moja au hawa watakuwa na sheria yao tofauti? Ndio swali langu. Wafungwa, na hawa ambao ni suspect, kwamba watakuwa na accommodation nzuri, na mavazi mazuri na chakula kizuri, je hawa ambao washapatikana na hatia tayari hata wakafungwa sheria itakuwa ni hiyo hiyo ama watakuwa na sheria yao tofauti?

**Joseph Mkuzi :** Mimi ni Geoffrey Mkuzi kutoka Rabai. Tumezungumza habari ya hali ya wafungwa kuwa nzuri au suspect kuwa watajukuliwa katika hali ya kibinadamu ya sawa. Lakini sasa ikiwa hawa watu tunawathania au ni wafungwa au bado wanaenda kortini watachukuliwa katika hali nzuri, wale waliumizwa victims now wana haki gani katika Katiba watachukuliwa nao watabembelezwa vipi, watafanyiwa restituion ya properties zao na maumivu yao vipi na Katiba?

**Daniel Munga :** Kwamajina naitwa Munga Daniel natoka hapa kaloleni. Swali langu au mswada wangu ni kuhusu human resource development. Mmezungumzia kuhusu elimu ya bure katika shule za msingi na kupunguzwa kwa karama ya elimu. Ninavyojuu elimu inaweza ikawa ya bure lakini pia ikawa haifai. Na hapa hatuoni kwamba mbali na hiyo elimu hiyo ya shulenii pia tunaangalia kama vuo hivi vya ufundi, mbona kuwa mtu akaweza akapata ujuzi wa kutosha na itaangaliwa kivipi? Ninauliza hivi, ya kwamba kuwe na Constitutional, au kuwe na hali ya kuwa Katiba ina mwelekeo wa watu kuwa wanakuwa wafanyi kazi wazuri kwa sababu maendeleo haiwezi kupatikana ikiwa wafanyi kazi sio wazuri. Na tena nataka niongezee pale kwa elimu ya kwamba kuwe na kuajibika kwa wale viongozi kama kutakuwa na vipengele vya kuwafanya wao pia wawe na kuhusika zaidi kusikia uchungu na ile elimu ambayo inaendelea zaidi ya kuwa tu ni mwananchi wa kawaida. Kwa mfano hivi sasa watoto wako nyumbani lakini kama mwenzangu alivyosema ni kwamba kuna wengine wanasoma na hata hawa viongozi watawala, wacha niwaite watawala wetu, watoto wao wanasoma nje kwa hivyo ni sawa hata wakikaa nasema watoto warudi mwaka ujao. Kwa sababu watoto wao hawako pale nahana hali tunaweza tukajitetea kikatiba unaona tungkuwa na njia moja kuwa hawa wakiwa elimu inaharibika wanasikia uchungu na pili sisi tuwe tuna njia ya kujitetea kikatiba kama hawa watu hawatupati elimu ile ambayo tunatake na tena tuhusishwe wakati mfumo wa elimu au in the designing of the curriculum. Tuwe tunahusishwa watoto wetu watafundishwa kule tuwe tunajua ya kwamba mtoto wangu akienda shule atafundishwa hivi na vile na hivi, lakini si watu kule wachaguliwe tu tuambiwe ni 8-4-4 na sisi tunaenda 8-4-4 hali hawa watoto wao wanapelekwa wanawapatia elimu ingine. Asante.

**Constance Mwamzi** :Mimi kwa majina naitwa Constance Mwamzi kutoka Kambe Location. Swali langu ni kwamba naulizia kuhusu wale watumia ambao wako kule National Assembly, ukasema ya kwamba watu 30 inasemekana wawe kina mama, wale wamama watachaguliwa kivipi na kielimu ni kivipi, na umri pia? Nilikuwa nataka nielewe kutokana na hayo. Asanteni.

**David Wachira** : Kwa majina ni David Wachira, mimi ni mfanyi kazi hapa na ningetaka kuuliza vile nilisikia tu kama wafanyi kazi wote wa Serikali ile muda wao wa kuhudumia wananchi ni miaka kumi. Hii kama itatumika kwa wafanyi kazi wote wa Serikali ni waalimu hata civil servants kwa sababu maoni yangu ingefaa hizi kazi zifanywe na Contract kama kwa waalimu ama hata civil servants, ili ukitaka kutoka after 10 years unatoka na unapata maruburubu yako ya mwisho. Na pia kama sasa hivi ambao umeshaajiriwa unatakiwa ufanye kazi mpaka miaka 55 na kama utatoka kabla ya hiyo miaka yako, sasa itakuwa wewe mwenyewe umepoteza yale maruburubu yako. Kwa hivyo mimi ningeona iwe kwa contract.

Na ya pili nataka kuuliza kwa Katiba hii traffic rules ama sheria za barabara ziko wapi? Mwisho.

**Stephen Katumo Kavu** : Mimi kwa jina naitwa Stephen Katumo Kavu kutoka Rabai, nataka kuuliza hii Katiba hapa inazungumza habari za District lakini kuna mahali panazungumza concurrent list yaani, revenue hupatikana. Wanataja kitu kodi, kodi hili linasemekana litakatwa shauri ni Central government halafu lipelekwa kwa District. Kwa wakati huu wa Kenya tunatoa kodi ya indirect sio kodi hiyo ya straight ambalo lilo la ukoloni tulilopata kwenye enzi za zamani. Sasa hapa halikueleza sawasawa, hili kodi litakuwa la such colonialist system au litakuwa kodi la aina gani? Pili hawakueleza pia ni percentage gani ambao itawachwa kwa district kwa location, kwa village, ya ile kodi itakayokusanya.

Swali lingine ni kifungo cha 42 cha slavery and servitude, wanasema no person should be forced to do forced labour. Ile IPPG ya mwaka 1997 iliondoa habari za harambee ya lazima. Na hapa haikuelezwu tunataka tuchanganye tujue je hii forced labour yiko namna gani, kwa sababu harambee pia ni indirect forced labour.

**Reuben Tsumah** : Bwana Commissioner sijui nitaanza kivipi lakini utaniwia radhi maana yake nimekuja hapa kusikiliza wenzangu kutoka Kaloleni kwa yote yale ambao wamesema. Mimi ningeomba, either kama ni hivi sasa unipe nafasi kidogo I want to make a statement, ambayo is a text ambayo iko prepared juu ya shuguli za leo ambazo zinaendelea.

Nataka niwaeleze kwanza shilingi ina pande mbili na tuzije tukasahau kwamba shilingi upande moja ni portrait ya Mzee upande mwingine ni Crown, nataka mshikilie hilo jambo. Nataka pia mshikilie kwamba tangu tulipopata uhuru mpaka leo karibu miaka thelathini na tisa na ninataka mchukulie leo kwamba kwa miaka hiyo tumekuwa katika kipindi ambacho kimeendeshwa na Serikali aina ile ambayo tumekuwa mpaka leo. Nitasonga mbele.

We the people of Coast Province in particular from Kilifi District wish to make our contributions and observations on the Draft Constitution as follows: The Review Process of the Constitution of Kenya wa first and foremost

**Interjection :** (inaudible)

**Reuben Tsumah:** Basi nitakwenda katika text yangu kwa njia ile umesema. Ni hivi Bwana. Tumesikiliza mengi hapa lakini kitu ambacho ningetaka mafanua kutoka kwa Draft Constitution, mtuelezea kama Katiba hii maana yake hii Katiba yetu, hii Draft Constitution yenu haikutaja kama Kenya is a Parliamentary or Presidential Republic. Na mimi nafikiria kuna muhimu, maana yake kukiwa ni Parliamentary System, the President is purely ceremonial while the Prime Minister is a general Manager. Kwa hivyo hatutaki kukombanisha President na functions za Prime Minister. Vile ambavyo tungetaka ni kuondoa shida hizo. Na isitoshe kama mingetangulia kusema, tumekuwa katika experiment ya unitary government kwa miaka karibu 38 na sasa kama nilivyo tangulia kusema shilingi ina pande mbili. Jamanini mimi nimesema hii Draft Constitution na wengine wengi, Wakenya wengi, lakini vile ambavyo mimi nimeona ni kwamba tunawekwa katika kipindi kingine cha experiment. Na hiki kipindi kingine cha experiment mimi kwa maoni yangu na maoni ya wengine, ni kwamba hatutaki kuregeshwa tena katika hali ambao tumekuwa kwa miaka hii thelathini na minane. Tunataka Katiba ambayo itafafanua haki ya mkenya. Nitazonga mbele.

Sisi au mimi ningependelea a Federal System maana yake a Federal System.

**Com. Swazuri :** (inaudible)

**Reuben Tsumah :** Okay basi wacha niyafupishe. Sijui ni kifungu gani lakini ningetaka kuzungumzia kuguzia tu kwenye land. Land belongs to the communities and it does not belong to Kenya. Umeeleza hapo? Basi kama ni hivyo wacha nisije nikachukua muda mrefu, mimi nafikiria vile nitakapofanya ni kwamba baada ya haya yote nitakukabidhi kama Commissioners hii memorandum ile yale ambayo pengine yatakuwa haikutajwa hapa, utaweza kuichukua.

**Com. Swazuri :** Pole Bwana wajua tumekutatiza kwa sababu wakati wa mwanzo tumeeleza taratibu za mukutano huu. Na leo tumekuja hapa, maoni tumeshachukua sasa tunataka reaction. Ngoja tujibu haya kwanza halafu tutakuja kwa hayo.

Councillor hapa anasema kwamba tunataka tupewe muda zaidi tuisome halafu ndio turudi hapa ndio mtupatia, hiyo ni sawa. Baada ya sisi kuondoka leo hapa District Coordinator atampanga watu wa endeleo kuchangia huu mjadala. Haikuletwi ili mwiangalie tu hivi, imeletwa mujadili ambapo ni sawa mseme, pana makosa mweleze hapakuwekwa mseme. Hiyo ni sawa.

Elimu ya madiwani na umri wao ni kweli haikuelezwa wazi hilo ni kosa kweli. Lakini tu tumeeleza katika general principles ya kwamba viongozi wale ambao wataenda kwa Bunge wawe lazima ni Form Fours, kuna mama ambaye ameuliza kuhusu kiwango cha elimu cha wale watu wa National Council. Wale 100, wale lazima wawe Form Fours. Lakini kwa hawa wengine nafikiri imekosekana hapo.

Halafu Katiba itaanza kutumika lini? Kulingana na sheria yetu sisi tukisha toa mswada katika Bunge, ile siku ya kwamba mkuu wa sheria amechukuwa mswada wetu halafu ukaenda Bunge, halafu wakimaliza ku-discuss katika wiki moja, ni lazima wapeleke kwa Rais atie mhuri na iwe ni Sheria, inaanza kutumika hapo immediately, unless wao warekebishe Katiba waseme sheria hii Katiba hii itaanza kutumika baada ya muda fulani lakini hiyo ni amendments ambao lazima wafanye kwa sasa ni akishatia ile sign ile basi tayari.

Halafu kuna swala la mvumo wa elimu, education curriculum hiyo Bwana Kalama ametoa mawazo kwamba lazima tuifanyie marekebisco, nafikiri hata hiyo ni sehemu moja ambayo bado tunaiangalia. Tumekubaliana kwamba elimu itakuwa bure, na ifanywe rahisi lakini ule mvumo ndio ambao hatukuweka ndani kwa hivyo ilikuwa imependekezwa tujue ni mvumo gani ambao utakuweko.

Halafu wakaja na swali la death sentence kwamba alieua lazima auawe. Sasa hapa tumesema kwamba aliuwa ni lazima auawe kweli lakini tumewapatia nafasi maana yake hizi prisons hat tukazibadilisha jina tuzita correctional ni kwamba wanaofanya makosa wanatakikana warekebishwe. Wanaofanya makosa hao ni binadamu. Tunataka kwanza wafanyiwe marekebisco kule kupelekwa jela kule ni kwamba pengine akitoka pale atakuwa yeye ni mtu mwema. Lakini ikiwa tutakuta kwamba ameua na hatuwezi kumtoa, basi afadhali akaishi maisha yake pekee yake lakini asiwadhuru watu tena ndio logic ambayo ilitufanya tukaweka life sentence badaba ya death, maana yake katiti sehemu moja tumesema life is sacred, lazima iwe protected.

Katiba na uchaguzi tumeeleza pale. Mawaziri tumeeleza vizuri sana kwamba mawaziri hawatakuwa wabunge na wabunge hawawezi kuwa mawaziri kwa hivyo ikiwa kuna mtu ambaye haweza kuhonga awe atachaguliwa kuwa waziri kuna free school hapa ya kwanza imesema kwamba kuanzia siku ya kuitisha Katiba hii tumepega marufuku corruption ya aina ye yeyote. Sasa itakuwa ni neno la Katiba siyo neno la sheria lile ndogo ndogo, ah, aha corruption ni hatia katika Katiba na wewe ukiona mtu anafanya corruption, una haki ya kumshtaki kwa yule public defender, Ombudsman au kwa Commission ambao tutaiweka ya human rights, wewe una haki na corruption ni hatia kwa anayetoea na anayechukuwa. Sasa ikiwa mtu atatoka akamhonge Mbunge ili achaguliwe awe waziri, huyo Mbunge tayari yeye ni corruption na ni ground ya kutoa yeye. Hizo sheria ambazo tumeziweke kwa hivyo ikiwa tutatokea watu ambao watakuwa na pesa wanataka kuwa mawaziri lakini wanatumia njia ya hongo hao tunajua kwamba hawatafaulu. Ikiwa tutafwata hiyo sheria yetu. Ingawaje wawezekana lakini twafwata sheria mpya haitawezekana.

Halafu wafungwa na wale suspect ndio watapewa treatment ya sawa hiyo maana yake tunasema tunawarekebisha hawa. Nikuwaadhibu ili wakitoka pale wawe wako sawa kwa sababu ile sheria ya mukoloni inaamini kwamba ukimshika mtu kama hujamfunga umuadhibu sana mpaka akubali makosa yake. Lazima alifanya hakufanya lakini akubali. Akisha kubali ni kwamba ameenda jela huo sasa ni atezwe kule ikiwezekana pia asirudi lakini asirudi naya awe amekoma. Hiyo ndio principle ilipokuwa ikitumika na mpaka sasa ni hivyo. Lakini tunasema siyo hivyo pengine mtu alifungwa kwa makosa pia yawezekana, na wengi hufungwa kwa sababu ya makosa ambayo yametokea hata katika uamuzi ule ndio maana tukatoa rufaa sasa badala ya kwamba

ufanya mtu atezekile tunasema aende kule akarekebishwe. Kama kweli ni mbaya huyo ni mwizi kule kule ataonekana. Kwa hivyo tunataka awa anaishi maisha ya sawasawa, lakini tu ni ile kwamba hana freedom kama vile wewe uko nayo sasa. Hawezi kuamua leo naenda Mombasa, kesho naenda kilifi. Lakini yuko katika area ile ile, lakini pale anakokaa anaishi maisha ya kibinadamu. Ni mwizi lakini hata yeye ni binadamu, hata yeye ana haki zake hii ndio tunasema ndio tofauti. Za hizi ukienda kutembelea ndugu yako ambaye huko jela saa hizi wewe ukifika pale wewe mwenyewe ukitoka walia vile alivyo. Pengine ulipomjua nyumbani alikuwa mkubwa namna hiyo tunaamini kwamba tukimtengeneze vile atakuta kwamba amerekebishika akirudi hapa atakuwa mtu wa sawa sawa.

Na wale victims now tunesema tusi-correct wale suspects, hata victims, ukiangalia katika bill of rights tumeeleza hii. Hata yule ambaye ameonewa naye pia compensation lazima ipatikane kwake. Kwa mfano mtu ameibiwa ng'ombe yake, yule aliiba ng' ombe tumefungua na yule mwenye ng'ombe, sheria inasema pia iangalie yule ambaye ngombe yake imeibiwa.

Halafu tunaenda kwa humam resource development umeeleza habari ya people to be responsible watu wajue elimu gani watoto wao watapata. Kama ni haya mambo ya waalimu ya migomo tujue na education system iwe inaangaliwa na wananchi. Hapo, wajua hapo bado kuna vitu hatujamaliza. Maana yake kuna zili Commission, Koech Commission tulitoa report yake bado tunaiangalia ile, ndio tuongeze na maoni ya wananchi ndio tuweke pale. Ni kama vile land, mambo ya land, Tume ya Land ya Njonjo haijamaliza mambo yake lakini tulichukua maoni ya wananchi tunaongojea ile pia tuchangishe pali kwa hivyo hili swala la elimu, Tatiary instititons na kadhalika pia litaangaliwa zaidi.

Mama ameuliza habari ya wale kina mama thelathini watachaguliwa vipi, wale wa National Council. Ni vile vile tunesema kama district, kila wilaya, kila mkoa utapewa nafasi nne direct. Kutakuwa na debe la kina mama bado, mwachagua mama ambaye atawakilisha mkoa wa Pwani kwenda kwa Upper House. Sasa wale wenyewe watajitokeza, ni campaign zao lakini majina yao yatatokea pale tutachagua wanne per province. Kwa hivyo mtachaguliwa na wananchi ili mbunge wako wamjua uliyemchagua.

Na ile miaka kumi. Bwana Wachira ameuliza habari ya contract, sikusema wafanyi kazi wa Serikali wawe na miaka kumi, ah, ah, viongozi wale wa uma. Elected leaders and appointed leaders by government or by Parliament kama wakuu wa Parastatals wakuu wa hizi commissions hao tumewapatia maximum tenure. Hawa wengine mpaka 55 ukitaka early retirement, yiko ground 40 years. Ukifika 40 years unachukua early retirement. Lakini hilo wazo lako la kwamba employment iwe kwa contract tutaliangalia. Lakini miaka kumi ni kwa wale elected leaders na wale national leaders kwenye Commissions na kadhalika, ten years.

Halafu ukauliza traffic rules, traffic rules sasa is a matter of detail. Najua waenda upande wa accidents na hongo lakini ile broad principle ya outlaw corruption tunesha iweka. Halafu broad principle of code of conduct ya wafanya kazi ipo, sasa details za kwamba askari akichua hongo tufanya hivi na hivi sasa itakuwa kwenya traffic act sasa.

Kodi – nakumbuka watu walisema 70% ibakie kwa local 30% iende kwa Serikali kwa hilo ni swala ambalo tutaliangalia tumeandika kodi tu, taxes itatozwa lakini hatukuandika ile percentage.

Halafu tumesema pia national government itachukua kodi halafu na district government, itatoza kodi halafu tukiweka sheria Wabunge pia national government itatoza kodi. Sasa vile viwango vitaenda wapi ndio hatujasitaja, lakini katika national government, tumesema kwamba lazima itapeleka pesa katika hizo sehemu zote. Itapeleka pesa kwa regional, itapeleka pesa kwa district, itapeleka pesa kwa location, itapeleka peza kwa village. Ingawaje wale nao pia watakuwa na uwezo waku-raise pesa. Hapo nakubali hatujaweka sawa sawa ni kina nani watatoa kiwango gani.

Forced labour umesema harambee ni forced labour nafikiri tumeondoa wale watu ambao walikuwa wakisemekana wanaifanya harambee iwe ni force tumeondoa tayari kwa hivyo sidhani kama itawezeka kulazimishwa watu, kushika kuku wa watu ili wafanye mchango wa harambee.

Bwana delegate hapa ameeleza kuhusu ile mixture ya Republican au Parliamentary system. Kitu ambacho tumefanya, tumechukua uzuri wa Parliamentary na uzuri wa ile nyingine. Hatukutaka kwenda extreme, either Presidential fully au Parliamentary fully upande wetu tumechukuwa sana France na Canada tumefwata fwata kidogo mifano hiyo. Maana yake ukichuku full republican sana ina taabu zake nyingi. (**end side B tape 2**).....

Council au nirudi kwa wananchi, kwa hivyo tumeweka safeguard, haya wengine? Nilikuwa nimesema ni yule Bwana kule.

**Valentine Matsaki :** Mimi kwa majina naitwa Valentine Matsaki Diwani Kambe. Mimi nilikuwa nataka kuongea kuhusiana na hawa mawaziri ambao si wabunge na nilikuwa napendekezo. Mawaziri wanaweza wakawa 15 lakini wakatoka mahali pamoja pamoja. Lakini mimi pendekezo langu ni kwamba kwa sababu tuko na mikoa minane basi katika wale mawaziri tuhakikishe kwamba kila mkoa tunaweza tukapata waziri pale. Na hata pwani tuwe na wawili kwasababu ni mikoa minane namba hatashikana vizuri.. Yaho ni mapendekeza yangu, asanteni.

**Stephen B. Mwajoha :** Mimi kwa majina naitwa Stephen B. Mwajoha. Kutoka Ruruma location. Mimi nataka nizungumzia juu ya hawa wafanyaji kazi utakuta kwa Katiba hii tulio nayo mtu mmoja anakaa kazi zapata hata sita. Huku utasikia yeze ni Chairman wa Board fulani tena yeze ni Chairman sijui Board gani tena mpaka yeze hata nakumbuka kuna bwana mwingine alikufa juzi juzi yeze alikuwa ni Chairman wa sehemu sita. Yeze ni Chairman, sasa mimi mapendekezo yangu nimeona kwamba kuna watu wamekaa tu hivyo hawana nini, kwa nini cake ile tuzigawe mtu mmoja apate kazi moja. Kama ni kuchaguliwa hiyo u-chairman, siyo mtu mmoja arundikiziwe u-chairman wa mara sijui sita, nane hii mimi naona hapo si sawa sawa. Asanteni.

**Kenga Kirao :** Kwa jina naitwa Kenga Kirao kutoka Kinani sub location. Swali langu ni kuhusu udungaji mimba. Inasemekana ya kwamba watungaji mimba wako lakini waoaji hakuna. Sasa nilikuwa naomba au nauliza ikiwa Tume

ilibadilisha meno la Majimbo kwa nini izitoe kitu cha kutisha hawa wadungaji mimba ili wakapungua? Hayo ilikuwa ni maoni yangu. Watoe jambo au kitu cha kutisha wadungaji mimba. Ili wakajua bure mtu moja anaweza dunga mimba wasichana kumi siku moja. (laughing) Thanks.

**Stephen Ngumbao :** Kwa jina naitwa Stephen Ngumbao. Nimeona mahali hapa katika Bill of Rights upande wa equality nimeona kwamba japo tunazungumzia equality, na ni haki ya kila mmoja awe na usawa na yule mwingine lakini nilipoendelea kusoma nikaona vipengele zingine za wanawake, watu wazima na watoto. Nikashindwa sasa mimi niko katika kiwango gani na ni mwanaume? Kwa hivyo nikaona kuna ubaguzi wa hali fulani hata ijapo kuwa kumeandikwa hapa kwamba kuna equality, lakini kumeandikwa women. Ingekuwa ni women and men ili kwamba isionekane kwamba zamani wanaume walikuwa na haki zaidi ya wanawake. Asante.

**Ngala Kibanzu :** Mimi kwa jina ni Ngala Kibanzu yangu ilikuwa ni suruwa kidogo ulipotaja hii 30%. Tume lilipo fika hapa sisi tulisema kila distribution iwe ni 10% lakini sasa hii 30% uliotaja hapo. Sisi mlipokuja hapa tulisema kuende huko juu 10% so that --- Ndivyo tulivyosema hapa.

**Interjection :** (inaudible)

**John M. Kassuku :** Asante sana Bwana Treasurer. Tumesikia hapa Bwana Commissioner ukatuambia ya kwamba ukiwa mbunge asiwe waziri na nakiwa waziri asiwe mbunge. Hiyo pia itaongeza nafasi za kazi zaidi. Swali langu ni hili, tulikuwa tunesikia pia kwamba anayetaka u-chairman wa Baraza asiwe Diwani, sijui ukweli huko wapi. Ni hivyo kwamba mtu akiwa Diwani asiwe, yaani akiwa chairman wa Baraza asipiganie u-diwani ama Diwani anaweza kupigania halafu akachaguliwa akawa Chairman wa Baraza.

Tatu, hawa ambao wame, hizi councils ambazo zimetajwa hapa utakuwa na malipo? Asante sana. Yah, zile za vijiji na location, kutakuwa na malipo? Asante sana.

**Shadrack Leo :** Mimi kwa majina naitwa Shadrack Leo kutoka Rabai. Nilikuwa nauliza mtufafanulie ama mtueleze vile Katiba ilivyo tungwa. Kama imelinda raia wa Kawaida kuhusiana na uchawi na huu uchawi wa Kizungu wa devil worshipping. Ambapo ni jambo kubwa sana ambalo linatatiza raia. Itakuwa kama MP nani lakini ukija kwako huna amani itakuwa si vizuri. Kwa hivyo utueleze pale Katiba imehusika kwa yale mambo ambao ni hatari kwa maendeleo ya raia wa kawaida.

**Abdallah Abayo :** Kwa majina mimi naitwa Abdallah Abaya kama nilivytangulia kutoka Mwanaminga. Saa hii ningependa kuchangia upande wa elimu kama tulivyoona mapendekezo ya wengi imeguzia kwamba elimu ya msingi iwe ya bure na kutakuwa na garama kidogo pengine za shule za upili hii inamaanisha kwamba idadi ya wanafunzi wataosoma itakua imeongezeka sana karibu kila mwaka. Serikali itakuwa ina toa wanafunzi zaidi kuliko ilipokuwa miaka ya nyuma kwa hivyo

ningependa kuuliza Constitution Review iangalie upande wa vio vikuu, anangalau kila mkoa upate uzawa wa kuwa na Chuo kikuu. Asanteni.

**Nzaro Makenzi :** Kwa jina naitwa Nzaro Makenzi kutoka Kaloleni. Naguzia kifungu cha 156 cha hii Draft Katiba. Kinaongea kwamba yule mkombeaji wa u-Rais awe ana shahada ya Chuo kikuu yaani degree kutoka University. Lakini swali ni kwamba je wale ambao hawana ma-degree na wao wamefanya pengine professional courses kama CPA Kenya, pia huyo naye awe ataachwa? Maoni yangu ni kwamba katika kiwango cha elimu hapa nafikiri kama itakuwa tu ni mtu ambaye pengine amefika Form Four na ana professional certificate na pengine iongezewe kwamba awe na proven administrative experience hapo pengine tutapata watu wengi Kenya ambao wanaweza kushikilia office hiyo. Asanteni.

**Tunje Eric :** Kwa majina najulikana kama Tunje Eric. Hoja yangu ni kuhusu elimu. Mimi ni mwalimu na nafikiri Bwana mwenyekiti umesema kuwa kuhusu elimu hamjajua haswa ni mvumo gani ambao utatumika. Lakini nafikiri tu juzi jusi tulikuwa na curriculum review ambao hata kulingana na vile ninavyojua implementation inatakitana iwe January 2003. Sijui hiyo itaitiwa katika elimu kulingana na hii Katiba mpya ama mipango hiyo itakuwa inaenda kimnagani. Kwa hivyo ningetaka pia Katiba mpya iangalie kuhusu lile jambo, kwa sababu inaonekana tutakuwa saa yote kuna mabadiliko, kwa hivyo wanafunzi pia wanatatanishwa. Asanteni.

**Cllr. Daniel Mwachinga :** Mimi ni Councillor Daniel Mwachinga kutoka Ribe. Mimi langu ambalo nataka nizizitize ni kuwa taifa lililo na msimamo ni lile ambalo lina tazama watoto wake vizuri. Ikiwa Katiba mpya haitaweka msimamo vizuri ya haki za watoto hata watoto watazaliwa tu wakitufa hivi hivi, kutakuwa na a lot of street children. Taifa hili litaendeleaje vizuri? Ninaona kuwa tuwe na mzimamo katika Katiba kuhakikisha kuwa watoto wa Kenya wakizaliwa wawe ni watoto ambao wana wazazi wawili, baba na mama. Lakini si sawa watoto ambao wanazaliwa na kupewa wazee kama sisi watunzwe na kazi yetu sisi tulimaliza. Tutakuwa tunaendesha nation ambayo haina msimamo. Asanteni.

**Taskaingu Chara :** Kwa majina nitajitambulisha kama Taskaingu Chara. Haswa kwa timu hii ambayo ni ya kurekebisha Katiba nashukuru kwamba imetaja mahali ambao tulikuwa tunaumizana sana. Hilo ni jambo la kwanza kuhusu administration ile kuanzia chief mpaka assistant chief. Hilo lilikuwa ni jambo ambalo tunatetana sana.

Pili tunataka tuangularie hasa mambo za ndoa. Ndoa za wakati huu tunapata kwamba mtu anafanya ndoa anaoa haijafikia miaka kama ya kuhesabu kama wanapata mtoto mmoja watoto wawili wanaachana. Hiyo tungeona kama wale ambao ni Kadhi ama ni wale ma-Pastors. Iwe kwenye Katiba kama ni kutoa certificate iwe imefikia kama umri wa miaka kama 30 wakiwa wanaishi pamoja. Na ingine tena watoto haswa kule kutengana na mama na baba haswa kwa wakati huu tunaona wanaumizana sana. Ingekuwa vizuri Katiba au sheria haswa iwe na kimila iingie hapo ndani iseme kama mila fulani ama kabilia fulani inataka hivi ni sawa kwa sababu Katiba itakuwa inaongezea uzito. Kwa kulinganisha tukisema ya nyuma ambao hivi sasa tunataka tuitoe, Mijikenda isikuwe na sheria yake na kusema haiwezi ikamwachia mwanimamke mtoto. Lakini kwa sasa tunataka tubadilishe.

Haidhuru lakini tungeongezea kidogo kwamba iwe itaweka kama sheria ya kwamba watoto wale wasiwe wanaweza kanyimwa kwenda kwa mzazi wa kiume ama kwa mzazi wa kike ama kuwa anatetanishwa na wale wazazi wawili. Tuwe tuna unguvu wa umoja ya kwamba akiwa amezaliwa na baba na mama wameoana. Ikifika mahali ambapo wamapewa kibali ama hata hawajapewa lakini wametoana mahari ni kuamisha kwamba wamethibitisha wameoana wamekubaliana kuishi, angalao iwe na uzito wa wale watoto wazitetenishwe wakapata uzito kwamba hawajui baba ni yupi hawajui mama ni yupi. Ninaonelea –

**Cllr. Munyachi :** Mimi ni Councillor Munyachi labda swala langu nilozungumzia ni kuhusu hawa ma-ministers pamoja na MPs pengine kuna mvumo gani ambao utamfanya yule minister ambaye atakuwa amechaguliwa pengine anatoka Pwani au ye ye ana vested interest za ye ye pengine asimamiye ubunge kiasi cha kwamba watakuwa na clash pamoja na yule mbunge wa ile area, ile ionekana labda mmoja anam-undermine mwenzakie waziri hafanyi vizuri kwa sababu ya yule mbunge ama mbunge hafayi vizuri kwa sababu ya waziri kwa hivyo mapendekezo yetu ni kwamba pengine yule waziri atakachaguliwe awe hatakuwa na matarajio kwamba atakuwa mwana siasa baadaye, kwa hivyo asiwekwe pale kumtatiza yule mwanasiasa ama mwanasiasa amtatize yule waziri. So that kama ni mambo yaendelea sawa sawa.

Na swali la pili sijui hayo mambo ya mawaziri 15 kutoka nje, it is either, ilikuwa imepangwa kufikiria kupunguza coping ama ni swala lipi. Kwa sababu nikipata kama kutakuwa na wabungu wanalipwa, mawaziri wanalipwa tutakuwa na watu wengi wanalipwa na hiyo fund ya kutokana na consolidated fund. Kwa hivyo sijui ni cost cutting ama ni kitu gani ambacho kilikuwa kimefikiriwa ile kwamba ionekana tusiwe na watu wengi wanalipwa wanafanya kazi ambazo kuna wengine walikuwa wanaweza kuzifanya. Hayo ndio .....

**Gideon Konde :** Kwa majina naitwa Gideon Konde nilikuwa na maswali mawili nataka kuuliza. Mtanisamehe nimekuja kuchelewa kidogo sijui kama yalisemwa. Kwanza ni upande wa elimu. Yamesemwa mengi lakini kuna elimu ya watu wazima nafikiri Katiba haikuguzia. Nilikuwa nauliza pengine ilikuwa imeachwa kwa mipango fulani, ama ni hali ya kusahau tu.

Pili, ni kuhusu citizenship. Sijui katika Katiba hii mwananchi atalindwa kivipi maana yake kama tulivyoelezwa inatakikana kuwe kuna identification, wakati mwagine mwananchi anaweza kuwa anatembea lakini hakubeba identification ye yote lakini kulingana na Katiba ya huko nyuma wananchi walikuwa nakipata shida sana kama hana identification na walikuwa wakipata matatizo na security wetu kwa kushikwa wakitembea bila identification. Na wengine ilikuwa inawafanya mpaka wakapelekwa jela. Sijui Katiba hii inaangalia kivipi kuhusu sehemu hivyo.

Pia wale ambao hawana kazi utakuta pia wao walikuwa wakipata matatizo kwa upande wa security wakishikwa wanaambiwa wanarandaranda ovyo na hali ni tu kwa sababu mtu hana kibarua. Sijui sheria pia inaangalia kivipi kuhusu mambo hayo. Asanteni.

**Patrick Kamoti :** Mimi kwa majina naitwa Patrick Saburi Kamoti Diwani wa Mguu Mwapata. Swala langu hasa lilikuwa

ninalenga kuhusu wafanyi kazi. Sijui ni mvumo gani ambao Katiba pengine imewaangalia hata kutetea haki zao kwa matajiri. Tuna mfano wa makambuni ambao huajiri watu vibarua zaidi ya miaka kama tano hata saba na mfanyi kazi akitetea haki yake kwa tajiri kumuuliza aajiriwe anafutwa sijui Katiba imeangalia vipi hapo. Na mfanye kazi yule yule kama ana haki anaweza kutetea kwa tajiri, njia aliyokuwa akitumia zamani ni mgomo. Mgomo sasa umeharamishwa. Sijui ni njia gani hasa Katiba inaangalia haki ya mfanye kazi kwa tajiri wake jinsi ya kujitetea. Ni hayo tu.

**Stanslaus Malau :** Kwa majina naitwa Stanslaus Malau. Ningetaka kuongea mambo mawili. Mwanzo kuhusu orphans. Kuna watoto ambao wameachwa na wazazi. Wako huko mashambani ndani ndani huko, sijui kama Katiba itachukulia uzito gani wakichagua makuzo yao ndio anapata a lot of support kwa sababu most of the parents wanajua hawa watoto wengi hawana hata uwezo.

La pili, ni kuhusu mtoto aliyetoka Standard Eight. Amepata elimu yake mpaka Standard Eight lakini bado hajakuwa self reliant, hawezি kujitegemea bado, sijui kama mzazi wake anaposhindwa kumpeleka Secondary kama kuna makadirio gani ambayo Katiba itawekeya kuhakikisha huyo mtoto baadaye anapata kujiendeza. Ni hayo tu Asante.

**Com. Swazuri :** Bwana Valentine anauliza habari ya mawaziri. Ukiangalia katika vile broad principles ambazo tumeeleza ni kwamba kila kundi la watu linalo chaguliwa kitaifa ni lazima liwe na Regional diversity. Hizo tumeziwaka hapo mwanzo kabisa kwa hivyo hapo ndani kila kitu kinachofanyika hapo ni lazima kiangalie ile, regional, religious na jinsia. Kwa hivyo kama ni Tume zinachaguliwa lazima ziangalie hivyo, kama ni mawaziri wanachaguliwa lazima waangalie hivyo, yaani hatutaki chombo cha kitaifa kiwe kina milkiwa na watu fulani. Hiyo iko ile broad principle. Kwa hivyo wale mawaziri kama ni 15 at least kila mkoa uwe na mtu mmoja au wawili ikiwa province moja itakuwa na waziri moja zile saba zitakuwa na wawili wawili province moja itakuwa na waziri mmoja katika assistant ministers itapata saidi, at least tuwe na balance. Siyo kwamba watoke sehemu moja. Hilo liko tayari tumeshaiweka.

Halafu mzee Stephen ameелеza kuhusu one man one job yaani mtu moja afanye kazi moja. Hiyo kweli tuliangalia sana lakini tukakuta kwamba katika kazi ya kuandikwa ndio atafanya kazi moja lakini kazi za kuchaguliwa mtu anachaguliwa kulingana na uwezo wake wakufanya kazi. Sasa utakuta wananchi wenyewe wameulizwa je mnataka nani wanasema ni fulani kwenya shule hii mkienda shule ingine wanaulizwa je mnataka nani wanasema yule yule maana yake ana uwezo sasa tukisema kwamba tunamkatia yule itakuwa kama tuwadhulumu watu wenye vipawa fulani na fulani. Kwa hivyo utakuta hiyo tuliwacha hivyo hivyo.

Halafu kuna swala la, mtu mmoja tuliona amesama mambo ya kudunga mimba tuondoe lile neno sijuia atasema tuweke lingine, ile hawa watu wapatikane na, watiwe ndani au wawe responsible kwa wale wasichana. Nafikiri ni swala ambalo bado linaingilia upande wa children's Act na upande wa responsibility of the citizen, kwa hivyo ukiangalia hivyo itabidi lazima tumewapa sheria ya Bunge kwamba Parliament watengeneze sheria ambayo itawalinda hawa wasichana. Au kuwa-punish wale wavulana au wanaume ambao wanatia wasichana mimba halafu wanawacha. Hiyo iko lakini yakiko directly kwa hivyo

tutaiweka iwe open.

Halafu Bwana Stephen naye pia akaeleza habari ya equality, women and men, ni kama kwamba huko nyuma ilikuwa ni wanaume, mpaka sasa wanaume bado, nikisema all Kenyans huwa wanaume kidogo ndio mambo yao yaangaliwe sana. Kwa hivyo hii ni kutilia mkazo tu kwamba itakuwa siyo wanaume peke yao siyo ‘he’ pekee yake ni he/she.

Tax 10% hiyo ni pendekero umetoa tutaliangalia lakini moja ameuliza kama yule Chairman wa District Council atakuwa ni Councillor, hapana, Chairman atachaguliwa na wananchi. Wale ma-councillor mtawachagua kama kawaida lakini yule atakayekuwa District Governor au District Council Chairman huyo naye atataka kura zake mbali, kwa hivyo ni vile vile kama mbunge hata kwa waziri hata kwa Chairman.

Halafu tukawa na habari ya uchawi na devil worshipping nafikiri hiyo hatukuweka, habari ya uchawi labda tukaangalie zaidi.

Halafu moja amependekeza kila mkoa uwe na Chuo kikuu, hiyo ni sawa.

Moja akaeleza kwamba si sawa kusuma kwamba Rais awe na degree. Tumejadili sana hiyo tukakuta hiyo ni lazima. Habari ya professional qualifications au experience haitoshi. Tunasema ni lazima awe na shahada. Kwa sababu anasimamia watu ambao wote watakuwa wamesoma viwango via juu. Sasa kama yeze ni Standard Four, halafu watu wote pale, mawaziri wote ni madakta na nini na nini atawaambia nini? Haiwezekani, hapo lazima tukubali haiwezekani. Wewe umeenda kwa mkutano wa Cabinet wewe ndio ulifika Standard Two wale wote wana ma-degree utawaambia nini? Hata kama ukiulizwa maswali mawili matatu, u mkali kabisa oh, mimi nimesema hivi. Umesema vipi? Huwezi kueleza. Kwa hivyo tumeondoa hiyo kabisa haiwezekani lazima awe na shahada.

Education system – ni kama vile nimeeleza tuna hii Commission nafikiri mambo yake yana—wewe u mwalimu unajua – yanakuwa implemented pole pole quietly. Kila siku unaona wameleta mambo mapya ambayo yako katika ile Tume lakini haisemwi kama yatoka katika ile Tume. Kwa hivyo tunakubaliana na wewe kwamba education system na tumeandika hapa isiwe inabadilishwa, badilishwa ile. Kila mwaka kuna nyingine. Hiyo tumekubaliana.

Mzee moja amesema watoto tuangalie tuondoe watoto nje ya ndoa. Kuna sheria za dini wacha hizi za wananchi hapa. Kuna sheria ya dini ambayo yasema haitakikani hiyo lakini mwanadamu pia amekiuka hiyo tutakuja kwa hii ambao tutatengeneza sis wenyewe. Ni neno ngumu sana hilo, kulifanya mpaka liziwe kwamba watoto wazitoke nje ya ndoa. Hiyo tutawachia Mungu sasa. Huyu ndio atawaadhibu hawa.

Halafu tena akasema tuhakikishe kwamba ndoa zinaishi miaka mingi. Sasa hiyo inategemea mafunzo na mila. Tabia na desturi za watu wenyewe wakisema wamekosana Katiba haiwezai kuwaweka pamoja wale kama wamekosana wamekosana hatuwezi

kuwa njia ingine lakini tu katika Katiba tumeandika ya kwamba tunataka kurudi ile miaka ambayo family ilikuwa ndio principle institution, kwa sasa family nyingi zimefurukika au watu wanakuta haina haja kuwa na family ndio tuko na hizo ‘come we stay’ kwa sababu hawaoni haja. Family yiko mambo mengi ambapo ukitaka kuwa na family lazima ukubali kuna mambo fulani huwezi kuyafanya kuna mambo fulani hayawezekani kuifanya. Sasa kwa vile watu wanataka urahisi, hawataki, lakini Katiba imerudisha imesema kitu muhimu ni family.

Halafu moja akauliza pale Councillors kwamba ministers ambao siyo wabunge. Tumesema wale ministers Constituency yao ni nchi nzima kwa hivyo si sawa kama tutawapatia constituency ya Kaloleni halafu tena na Constituency ya Kenya nzima. Hilo kwa binadamu haliwezekani. Tumejaribu kulijunguza lakini kuna either moja ataumia either mtu wa Kaloleni ataumia au Mkenya mwengine aliyo Migori ataumia sasa ndio tukasema wasiwe ni wabunge. Lakini huwezi kuwazui wabunge, mtu ambaye ame-serve kuwa waziri miaka kumi hakuna sheria inamzuia kwamba akimaliza miaka kumi asipiganie ubunge. Pengine atakuta kama nimefanya kazi nzuri wananchi wangu wamependeziwa nyumbani na mimi nitapigania ubunge sasa.

Halafu pili kazi ya waziri kama anaifwata vile tumepanga hapa hatakuwa hana time ye ache agongane nyumbani na mbunge wake. Kazi yake ni za national duties, yeye ni waziri wa Kenya nzima aangalie masilahi ya Kenya nzima ikiwa hapa nyumbani kuna shida ya maji na wewe ni waziri wa maji atakaa na mbunge wa sehemu ile na District Council and Village Council wapange lakini siyo kwamba ache amwinglie mbunge. Yeye anasehemu kubwa ya ubunge wa taifa nzimba kwa hivyo tuliweka hivyo kwa sababu ya kazi ifanyike vizuri siyo kwa sababu ya harama. Mnajua harama ni nyingi ikiwa mawaziri siyo wabunge harama ni nyingi lakini tulisema demokrasi mzee na tuko tayari kuiridhia lakini watu wawe wanaridhika.

Adult education – Ni kweli hilo swala tulilishau tutaliweka.

Halafu harassment ya wananchi kuhusu vitambulisho, tumeondo hiyo, katika Bill of Rights tunesema mwananchi hana haki ya kudhulimiwa, kurakiwa, kuulizwa lolote, na mtu yeyote. Freedom of movement, iko hapa na ikiwa yule askari atakuuliza kitambulisho tunesema ni lazima ata-identify ye ye mwenyewe ni nanai na kwa nini akuzuia. Lakini huwezi kusimamisha hapa watu kumi uwaambie leteni vitambulisho kama hamna shilingi mia mbili hapa mara moja. Hiyo tumeondo maana yake kuna freedom of movement, na freedom of association, na freedom of expression, zote ziko hapa.

Wananchi wasiyo na kazi tuliangalia sana swala hili tukakuta kwamba hali ya uchumi sasa haiwezi kuilazimisha Serikali kwamba wale ambao hawana kazi iweze kuwalisha, tulikuta hiyo haiwezekani. Lakini ikiwa siku zijazo itatakikana basi wananchi wenyewe mtasema katika referendum ili tubadilishe hiyo.

Na yule aliyesema kuhusu wafanya kazi. Haki za wafanya kazi ziko, ukiangalia katika bill of rights. Migomo bado iko. Nitakusomea hiyo ya wafanya kazi. Ingawaje maswala mengi ya wafanya kazi nimesema hakuyaandika vizuri lakini haki zao bado tuko nazo hapa. Ukiangalia kifungo number 55 kinasema kwamba : Every worker, kila mfanya kazi ana haki ya mshahara

mzuri, hali ya kufanya kazi nzuri, ana haki ya kujiunga na chama chochote cha wafanya kazi, Trade Union na ana haki ya kugoma. Ziko hapo number (d). Kwa hivyo hatujaziondoa zile haki za wafanya kazi.

Halafu mtu wa mwisho ameeleza habari ya orphan children, au watoto ambao wanatoka kwa jamii maskini. Tumesema kwamba ni jukumu sasa la Serikali lazima ilée watoto, maana yake kama tunesema lazima wapatiwe elimu ya bure na ya lazima sasa hilo ni indirect kuambiwa kwamba Serikali ni lazima ifanye majukumu hayo.

Na ukaeleza habari ya watoto wanatoka wa-drop out, shule. Tumesema kwamba kwa elimu ya Secondary School ifanywe rahisi na tunesema kwamba bursary ziwe zinapatika kwa wale wanafunzi ambao wanatoka katika jamii ambazo ni masikini.

Nafikiri kwa hayo machache na mengi leo tutakomea hapa na tunawashukuru sana. Nawashukuru vile ambavyo mmejitokesa kwa wingi lakini tunawapatia nafasi bado mweende mkakae Bwana Co-ordinator na watu wake wa 3Cs members watapanga mikutano sasa zaidi ya kila sehemu ili bado tunataka tupate mambo mengi mtatujulisha baadaye, mambo mengi ambayo mnataka kutueleza.

Ulikuwa unataka kuuiliza? Utapata nafasi.

**Trikonde :** Mimi naitwa Trikonde natoka Maweza. Pendekero langu lilikuwa ni kwamba hii Katiba ikiwa tayari zile nakala ziweza kutosha ili kila kijiji, ama ile vijikazo za vijiji ziweze kupata hizo vitambu. Kwa sababu kuna wengine hata ili Katiba ya zamani hatujui kwa hivyo vitabu tuwe tutazipata.

**Com. Swazuri :** Hiyo ni rahisi, mkitaka information tutaleta. Na tena nakala za Kiswahili zitakuja wiki hii. Niko tayari nakala za Kiswahili.

Kwa hivyo mtu moja atuombee tufunge. Nani atatuombea

**Emmanuel Baya :** Haya tufungeni macho. Mwenyezi Mungu Baba tunakushukuru mchana huu wa leo kwa kuwa umetutuliza mahali hapa kujadili mambo ya Katiba yetu ya nchi hii. Tunasema asante Bwana kwa maana tumeendelea katika utulivu hata Bwana tulifikia kilele.

Twakushukuru kwa sababu umetupa utulivu huo na yote ambayo tumeweza kuiongea Bwana tunahitaji ukaipikie mhuri wewe mwenyewe ile Bwana yakaweza kutekelezeka kiasi cha mwananchi aweze kuishi katika hali ya amani.

Tunasema asante kwa sababu utazidi kuwa pamoja nazi hata kwa ajili ya wageni ambao wametutembelea Bwana kapate kuzidi kuwa pamoja nao wape hekima zaidi ili Bwana kazi hii iweze kuendeleza katika hali ya usawa. Twakushukuru kwa sababu utaoneka akayatenda hao kwa sababu ni mapenzi yako. Kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

Kwa jina naitwa Emmanuel Baya kutoka Kaloleni.

The meeting ended at 2.45 p.m.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&